**8 JUNI, 2026**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

### Kikao cha Arobaini na Tano - Tarehe 8 Juni, 2026

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Yagi Maulid Kiaratu, Mbunge wa Singida Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 530

### Kuongeza Bajeti *TARURA* Manispaa ya Singida

**MHE. YAGI M. KIARATU** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaongeza bajeti ya *TARURA* Manispaa ya Singida kwa kuwa ni ndogo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Yagi Maulid Kiaratu, Mbunge wa Jimbo la Singida Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuongeza bajeti ya fedha za matengenezo ya barabara kupitia *TARURA* katika Manispaa ya Singida. Katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 bajeti ilikuwa shilingi bilioni 1.29 ambapo imeongezeka mpaka shilingi bilioni 1.35 kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027 bajeti ya barabara za vijijini na mijini katika Manispaa ya Singida imeongezeka hadi kufikia shilingi bilioni tatu. Aidha, Serikali imepeleka shilingi bilioni 24.75 katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami takribani kilometa 15.4 na soko la vitunguu kupitia Mradi wa *TACTIC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuongeza bajeti za ujenzi wa barabara za vijijini na mijini kote nchini ikiwemo Halmashauri ya Manispaa ya Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yagi, swali la nyongeza.

**MHE. YAGI M. KIARATU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ninaomba kuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Singida ni mji unaokuwa kwa kasi, lakini ni mji wa kimkakati kwa sababu uko karibu na Dodoma kwa maana hiyo ni mahali salama pa kupumulia Dodoma, lakini pia kuna ongezeko kubwa la watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka mitano Singida imekuwa ikihudumiwa mtandao wa barabara kilometa 523 tu, lakini kwa uhakika kuna zaidi ya kilometa 1,200 barabara nyingi ni mbovu kutokana na hali hiyo, barabara nyingi hazijafunguliwa na mimi kama Mbunge nimejitahidi mwaka huu nimeweka fedha za Mfuko wa Jimbo kufungua barabara, lakini ni kama nimechukua kikombe cha maji na kutia kisimani kwa sababu haigusi kabisa hali halisi iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya barabara ni mbaya hata barabara ya kwenda Ikulu Ndogo ambayo Rais ana...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa maswali sasa, maswali ya nyongeza.

**MHE. YAGI M. KIARATU:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu; ni lini sasa Serikali itafanya mrejeo wa kuona hali halisi ya kilometa ambazo zinahudumiwa ili ziendane na hali halisi ya bajeti inayopangwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuwafuta machozi wananchi wa Singida, nimuombe Waziri atutafutie hata kilometa tano za lami kwa sababu hizo fedha anazosema shilingi milioni 24 hazijengi kilometa 15 zinajenga kilometa saba tu. Kwa hiyo, bado kuna uhitaji mkubwa wa barabara za lami za mjini ili ziweze kuwasaidia wananchi wa Singida Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Singida Mjini Mheshimiwa Yagi Maulid Kiaratu, kwa ufuatiliaji wake wa mara kwa mara kuhusiana na uboreshaji wa miundombinu ya barabara katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua kwamba Manispaa ya Singida na Mkoa wa Singida kwa ujumla ni mkoa wa kimkakati, uko karibu na makao makuu, lakini idadi ya watu inaendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana katika kipindi cha miaka mitano bajeti ya kawaida ya *TARURA* imeongezeka kutoka shilingi bilioni 1.29 mpaka shilingi bilioni 4.35 lakini pia fedha za mfuko kwa kupitia Mfuko wa Benki ya Dunia *(TACTIC)* jumla ya shilingi bilioni 24.75 zimepelekwa kwa ajili ya kuboresha miundombinu.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutahakikisha tunakamilisha ujenzi, ukarabati wa barabara, zikiwemo hizi barabara za lami katika Manispaa ya Singida, lakini pili, nikuhakikishie tu kwamba tuko tayari kufanya marejeo ya barabara zinazohudumiwa na *TARURA* na huu ni utaratibu wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI nimwelekeze Meneja wa *TARURA*, Wilaya ya Singida na Mkoa wazipitie zile barabara muhimu ambazo zinahitajika kusajiliwa na kuingizwa kwenye mtandao wa *TARURA* ili zianze kuhudumiwa na *TARURA*. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Johannes Lukumay, swali la nyongeza.

**MHE. JOHANNES L. LUKUMAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nitangulie kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuongeza bajeti ya *TARURA* kutoka shilingi bilioni 944 na kufikia shilingi trilioni 1.2 kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Arumeru Magharibi lina changamoto kubwa ya miundombinu ya barabara, ninaomba kuuliza je, Serikali imetuongezea bajeti ya *TARURA* kutoka shilingi bilioni 2.3 ya sasa kufikia angalau shilingi bilioni sita hizi hizi barabara ambazo hazipitiki Malalua, Mlangarini, Nduruma na Bwawani, kuna Olgilai, kuna Barabara ya *Sokoni II* na Bangata, tuna Barabara ya *TPRA* kwenda Likamba, kuna barabara ya Mbauda – Losinyai, kuna barabara Kimamoto kwenda Mwandet, barabara ni nyingi sana na vivuko 135...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, amekwisha kuelewa.

**MHE. JOHANNES L. LUKUMAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali imetuongezea kutoka ile shilingi bilioni 2.3 mpaka angalau shilingi bilioni sita hivi hizo barabara ndugu yangu ziweze kupitika? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Johannes Lukumay, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi kwa ufuatiliaji wake wa mara kwa mara, lakini na mimi ninafahamu tulishafanya ziara katika Jimbo la Arumeru Magharibi miaka miwili iliyopita hali ya kijiografia na ardhi yake ya *volcano* inahitaji bajeti kubwa katika kujenga barabara ambazo zinadumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Lukumay na wananchi wa Jimbo la Arumeru Magharibi kwamba Serikali kila mwaka imeendelea kuongeza bajeti, lakini tunafahamu kwamba bajeti hiyo bado haitoshi kulingana na hali za kijiografia na ndio maana Serikali hivi sasa kupitia *TARURA* tuko hatua za mwisho za kupitia aina ya barabara za kujenga kulingana na hali ya kijiografia za maeneo husika ikiwemo Arumeru Magharibi.

Kwa hiyo, bila shaka tutakwenda kuongeza bajeti kuhakikisha barabara zetu zile zinajengwa na kudumu zaidi kutokana na hali za kijiografia za Jimbo la Arumeru Magharibi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Japhael Lufungija, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Ulyankulu wananchi wake walikubaliana kufungua barabara mpya kila kata barabara mbili kwa maana ya barabara 30 kwa maana ya kung'oa visiki na greda ya halmashauri kupitia Mkurugenzi na Mfuko wa Jimbo tumepeleka fedha kwa ajili ya kufungua barabara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini mpango sasa wa Serikali kuhakikisha kwamba barabara hizo zinaweza kujengewa kalavati ili zipitike kwa muda mrefu kwa kutimiza malengo ya wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mheshimiwa Lufungija, Mbunge wa Jimbo la Ulyankulu amefuatilia mara kadhaa kuhusiana na baadhi ya barabara ambazo zimefunguliwa kwa nguvu za wananchi, Mfuko wa Jimbo na fedha za halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nitumie nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, lakini nimpongeze sana Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kaliua kwa kutenga fedha za mapato ya ndani kuchangia nguvu za wananchi katika kufungua barabara na hili tumekuwa tumekuwa tukilisisitiza kwa Wakurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha pamoja na miradi mingine, lakini watenge fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya kuboresha barabara muhimu katika jamii katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge baada ya hatua hiyo ya wananchi kufungua barabara hizo na kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi na sisi Serikali Kuu tutafanya taratibu za kuzifanyia tathmini barabara hizo na kuzisajili rasmi kuingia kwenye mtandao wa barabara wa *TARURA* ili zianze kutengewa fedha rasmi kwa ajili ya matengenezo ya barabara hizo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali mafupi. Mheshimiwa Clayton Chipando, swali la nyongeza.

**MHE. CLAYTON R. CHIPANDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na barabara ya kutoka Mwanga kwenda *Airport* kuzibwa kutokana na Bwawa la Katubuka kujaa maji. Serikali ina mpango gani wa kuyaondoa yale maji ya Katubuka ili watu wa Mwanga waweze kwenda *Airport* kirahisi kwenye barabara hiyo ambayo ni ya lami? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba barabara kutoka Mwanga kwenda *Airport* katika Jimbo la Kigoma Mjini, Halmashauri ya Kigoma Ujiji ina changamoto kutokana na maji kutuama katika eneo lile la Bwawa la Katubuka na tayari Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kupitia *TARURA* tuko katika hatua za mwisho za kukamilisha hatua za manunuzi na kuhakikisha kwamba mkandarasi anakwenda *site* kwa ajili ya kudhibiti changamoto ya maji kutuama katika barabara ile ili tuweze kuikarabati barabara na kuwezesha ipitike vizuri.

Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Chipando na wananchi wa Jimbo la Kigoma Mjini kwamba Serikali iko kwenye hatua nzuri na tutahakikisha kwamba

tunadhibiti changamoto ya mafuriko ya maji na barabara ile iweze kupitika muda wote wa mwaka. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, nami niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunajua *TARURA* inafanya kazi kubwa sana, changamoto ni pesa hazitoki zote na kwa wakati. Katika Halmashauri ya Mji wa Bunda, bajeti iliyopita ilitoka 50% hivyo kusababisha wakandarasi kutolipwa na barabara kutopitika.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali mnatoa tamko gani kwenye bajeti iliyopita ili pesa zitoke zote kwa wakati, wakandarasi wapite barabara za Mji wa Bunda zitengenezwe ziweze kupitika muda wote? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Bunda Mjini dada yangu Mheshimiwa Ester Bulaya kwa ufuatiliaji wa mara kwa mara, lakini nimhakikishie tu kwamba bahati njema sana Mji wa Bunda uko kwenye Mradi wa *TACTIC* ambao utajengwa barabara za lami, taa za barabarani na miundombinu mingine muhimu sana. Kwa hiyo, Mji wa Bunda ni miongoni mwa miji ambayo inakwenda kuwa *vibrant* sana kutokana na bajeti ambayo imetengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba kupitia bajeti ya *TARURA* ziko fedha ambazo zimepelekwa kila mwaka wa fedha, lakini ziko fedha ambazo hazikupelekwa na Serikali mpango wake ni kuhakikisha kwamba tunapeleka fedha zote za bajeti kwenye miradi yetu na ikiwa hazijapelekwa katika kila bajeti ya mwaka unaofuata tunaweka utaratibu aidha wa kuongeza bajeti ili kuweza kufidia zile fedha ambazo hazijapelekwa. Kwa

hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali itaendelea kufanya kila aina ya jitihada kuhakikisha kwamba fedha za bajeti zinazopatikana ziweze kupelekwa kwa ajilli ya kuboreza barabara zetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana, pale Wilaya ya Muleba Mji mdogo wa Nshamba kuna mkandarasi alipewa *tender*, lakini kwa sababu za ndani mkataba haukusainiwa lakini barabara ni mashimo matupu kutoka Nshamba kwenda Bunyagongo. Je, Serikali itamruhusu lini huyo mkandarasi ili aweze kukarabati hiyo barabara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Nshamba katika Jimbo la Muleba Kusini kwa Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, ni moja ya barabara ambazo tayari Serikali imeshatoa maelekezo kwa Mameneja wa *TARURA* wa Mikoa na Wilaya kutangaza 60% ya bajeti kwa ajili ya kupata wakandarasi na zile ambazo tayari zina wakandarasi kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anasema kwa ajili ya kusaini tumekwisha ruhusu sasa hatua za kusaini mikataba ili wakandarasi waende *site* kwa ajili ya kwenda kufanya matengenezo ya barabara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Mbunge kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tutafuatilia kupitia Meneja wa *TARURA*, Mkoa wa Kagera na Wilaya ya Muleba ili barabara hiyo ipewe kipaumbele miongoni mwa barabara 60% zinazotangazwa au tunazosaini mikataba, mkataba usainiwe ili mkandarasi arejee aweze kwenda kufanya kazi ya ujenzi wa barabara hiyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mabula Magangila, swali la nyongeza.

**MHE. MABULA J. MAGANGILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Jimbo la Msalala ni jimbo ambalo lina shughuli za kiuchumi za uchimbaji, pamoja na kilimo na jimbo lile asilimia kubwa maeneo yake ni mbuga ambazo zinajaa maji kwa maana hiyo, bajeti ya *TARURA* iliyoko sasa hivi haitoshi na haiwezi kujenga barabara zile zikapitika kwa misimu yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni upi mpango wa Serikali kuongeza bajeti ya *TARURA* katika Jimbo la Msalala angalau kufika shilingi bilioni tano ili tuweze kujenga barabara zile ziwe kupitika kwa kiwango cha misimu yote? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Msalala na nimthibitishie kuwa katika kipindi cha miaka mitano kuanzia 2021/2022 mpaka sasa 2025/2026 kuelekea 2026/2027 bajeti ya *TARURA* mwaka 2021/2022 ilikuwa shilingi bilioni 250 kwa nchi nzima, lakini leo mwaka ujao tuna zaidi ya shilingi trilioni 1.2 bajeti imeongezeka kwa takribani zaidi ya mara sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii maana yake ni kwamba Serikali inatambua kwamba ziko barabara korofi, mtandao wa barabara wa *TARURA* umeendelea kuongezeka lakini dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba barabara zetu zinakuwa bora ziwe za lami na changarawe imeendelea kuzingatiwa.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunafahamu kwamba Jimbo la Msalala lina hali ya hewa ya mvua nyingi na maji mengi tunaendelea kuhakikisha kwamba tunaongeza bajeti na Msalala pia ni sehemu ambayo imenufaika na bajeti kuongezeka na tutaendelea kutoa kipaumbele katika halmashauri hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, swali la Mheshimiwa Onesmo Merdson Mnkondya, Mbunge wa Mbozi, litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Japhet Hasunga.

Na. 531

**Kukomesha Uuzaji wa Mbegu Feki Nchini**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA K.n.y. MHE. ONESMO M. MNKONDYA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kukomesha uuzaji wa mbegu feki nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa mujibu wa kifungu cha 15 cha Sheria ya Mbegu (Sura 308 Toleo la Urekebu 2023) mbegu zote zinazouzwa nchini lazima ziwe zimethibitishwa ubora na *TOSCI*. Ili kukabiliana na tatizo la mbegu feki, *TOSCI* inatoa lebo za kielektroniki kwa kampuni za mbegu ambazo zinamuwezesha mkulima kuhakiki uhalisia wa mbegu husika kwa kukwangua lebo hizo na kuingiza namba maalum kwenye simu yake ya kiganjani ili kupata taarifa ya kuwa mbegu aliyonunua ni halisia au siyo halisi. Matumizi ya lebo hizi yamepunguza tatizo la mbegu feki kutoka matukio 325 yaliyoripotiwa mwaka 2014/2015 hadi kufikia matukio 10 yaliyoripotiwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Serikali kupitia *TOSCI* inafanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maduka ya mbegu ambapo katika ukaguzi uliofanyika kuanzia Julai, 2025 hadi Januari, 2026 wafanyabiashara 13 wamebainika kujihusisha na matukio ya kuuza mbegu feki au mbegu zisizokidhi vigezo vya ubora ambapo mmoja kesi ipo mahakamani na wengine 12 uchunguzi unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nyingine Serikali imetoa elimu ya juu ya matumizi ya mbegu bora na namna ya kubaini mbegu feki kwa wakulima 5,822 kupitia kampeni ya mali shambani na wakulima 6,763 kituo cha huduma kwa wateja kwa maana ya *call center* waliopiga simu kuanzia Novemba, 2025 hadi Januari 18, 2026. Aidha, jitihada za kudhibiti uuzaji wa mbegu feki kwa wakulima ni endelevu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza niipongeze Serikali kwa majibu mazuri ya swali hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza; kwa kuwa, wakulima wa kawaida wa maeneo ya Igamba, Halungu, Itaka, Nambinzo, Msia, Isalalo, Iyula, Ipunga na Ihanga wanaelimu ya kawaida sana ya kuweza kutambua. Je, Serikali inatumia utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba wananchi wanazielewa hizo lebo za kielektroniki ili waweze kuhakikisha kwamba wanadhibiti hili suala? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa, uuzaji wa mbegu feki ni suala la uhujumu uchumi na kurudisha nyuma maendeleo ya nchi, na kwa kuwa watu hao wanajulikana vizuri na wamerudisha nyuma sana maendeleo ya wananchi.

Je, Serikali ipo tayari sasa kuwachukulia hatua kali wale wote watakaobainika wanauza mbegu feki ikiwa ni pamoja na kuwanyonga? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nikushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ili nimjibu Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mbunge wa Jimbo la Vwawa, ambaye ameeleza maswali yake mazuri, ya msingi sana na yenye

tija kwa wakulima wa Mkoa wa Songwe, jimbo lake, jimbo la jirani la Mbozi lakini kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza tu nimthibitishie kwamba tunaendelea kutoa elimu na kwa sababu tunajua jambo hili ni endelevu, tunaendelea kulifanya hivyo. Kwa hiyo, tutakacho kifanya katika maeneo kama ambayo ameyataja kule, Igamba kule kote unakwenda mpaka Itaka, kote kule tutahakikisha kwamba moja; tutawalazimisha sasa Maafisa Ugani wote, washuke kwenye ngazi za vijiji na kutoa hii elimu ya kutambua mbegu feki na mbegu halisia, ikiwemo, kutokununua mbegu yoyote ambayo haina lebo ya *TOSCI*, kwa sababu ile lebo kuna vocha ya kukwangua, ukishakwangua kuna namba pale chini ambayo unaituma na itakwambia hiyo mbegu ni *fake* ama siyo feki, kwa sababu zile namba zote zimekuwa *registered* kidijitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tutafanya hivyo ili kuhakikisha jambo hili linawafikia wakulima wengi na hasa wale wa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na kuhusu hao wanaohujumu uchumi, ni kweli na ndio maana unaona kama sasa hivi kuna kesi moja Mahakamani, wengine uchunguzi unaendelea na ninaamini baada ya uchunguzi tutawapeleka katika hatua hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, jukumu moja la Serikali kwa upande wetu sisi kabla ya matokeo ya kimahakama, sisi inakuwa ni kuwafutia leseni kutokushiriki katika hiyo biashara kabisa hapa nchini na katika biashara nyingine yoyote inayohusika na masuala ya mazao: kwa hiyo, hawashiriki kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hizo hatua za kunyongwa ni hatua za kimahakama, maelekezo sisi hatuwezi kuingilia muhimili mwingine, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa kuwa wananchi wa vijijini katika Mkoa wa Mtwara, walihamasika na kuacha kutumia mbegu za asili wakiamini mbegu zinazouzwa katika maduka zitaongeza uzalishaji lakini hali imeonekana sivyo ndivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ukiacha adhabu zilizotangulia kusemwa, Serikali haioni haja ya kutafuta namna ya kulipa fidia kwa wananchi wale wa vijijini katika Mkoa wa Mtwara ambao uzalishaji wao umeshuka kutokana na matumizi ya mbegu feki zilizotajwa kwenye swali la msingi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nimshukuru vilevile dada yangu Mheshimiwa Hokororo, kwa swali lake la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika maswali ya msingi, hatua ya kwanza ya Serikali imekuwa ni kuchukua hatua dhidi ya wale ambao wanauza mbegu feki lakini jukumu hili la msingi mtu wa kwanza anayepaswa kuripoti anapaswa awe mwananchi mwenyewe kwetu sisi na ndio maana unaona tuna *call centre* ambazo wakitupigia mapema, sisi tunawahi kuchukua hatua kwa wale wahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo suala la kulipa fidia, jukumu kubwa tumeanzisha mfuko wa *Agriculture Development Fund (ADF)* wenye lengo la kufidia maeneo ambayo tuona kunauhitaji wa lazima. Kwa hiyo, niseme tu katika eneo lako sisi tutakwenda tutafanya tathmini na kuona ukubwa wa hiyo changamoto ambayo imetokea, kabla ya hatua nyingine, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa, tunaendelea Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mbunge wa Chemba sasa aulize swali lake.

Na. 532

**Ukarabati wa Skimu ya Umwagiliaji – Kijiji cha Jogolo Kata ya Ovada – Chemba**

**MHE. KUNTI Y. MAJALA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakarabati Skimu ya Umwagiliaji katika Kijiji cha Jogolo, Kata ya Ovada - Chemba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, katika kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji nchini, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji katika mwaka wa fedha 2025/2026 inaendelea na utekelezaji wa miradi mitatu ya umwagiliaji ya Ndoroboni, Babayu na Skimu ya Umwagiliaji ya Jogolo katika Wilaya ya Chemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya miradi hiyo, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Mabwawa ya Ndoroboni na Babayu unaendelea na umefikia 30%. Vilevile upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Skimu ya Umwagiliaji ya Jogolo iliyopo katika Kijiji cha Jogolo – Kata ya Ovada umefikia 40% na unatarajiwa kukamilika ifikapo Oktoba, 2026. Baada ya kukamilika kwa usanifu huo, Serikali itaanza hatua za ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya miradi hiyo ili kuongeza eneo la umwagiliaji na kuimarisha uzalishaji wa mazao ya kilimo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tuzime *microphone* ambao tumewasha wengi, tupunguze.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Jogolo, ni mradi ambao ni wa muda mrefu sana, una zaidi ya miaka 27. Tumekuwa tukiomba fedha kwa ajili ya ukarabati wa mradi ule lakini ahadi zimekuwa ni nyingi na wananchi wa Kata ya Ovada wanautegemea sana kwa ajili ya kukuza uchumi wao, lakini na uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Waziri, mpo tayari wakati bado michakato hii mingine inaendelea, kutupatia kiasi cha shilingi milioni 60 ili tuweze kurekebisha miundombinu ya tenki pamoja na mifereji ili maji yasiendelee kupotea na wakulima wetu kukosa kabisa maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; Mheshimiwa Naibu Waziri, upo tayari kwenda Wilaya ya Chemba, kuzungukia miradi yote 17 ya umwagiliaji ndani ya jimbo letu ili Serikali muweze kuona ni namna gani mnakwenda kuimarisha miundombinu hiyo kwa masilahi mapana ya Wana-Chemba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nimshukuru Dada yangu Kunti, kwa maswali mawili mazuri ya msingi kabisa kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mahitaji ya eneo la Jogolo, walau wamesema wananhitaji shilingi milioni 60, siyo fedha nyingi sana. Nitazungumza na Mkurugenzi wa Tume, hilo lipo ndani ya uwezo wetu, ninaamini hiyo hela tunaweza kuipata kwa ku-*allocate* baadhi ya vyanzo. Kwa hiyo, tutafanya hivyo ili wakati hatua nyingine zinaendelea basi wananchi waweze kuendelea kutumia ule mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kwenda Chemba ni karibu sana, ni mwendo wa nusu saa tu hapa, nipo tayari twende *weekend,* hapo tupige kazi hapo halafu turudi, nitatembelea miradi yote na nitaifikia, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Mheshimiwa Exaud Kigahe, swali la nyongeza.

**MHE. EXAUD S. KIGAHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa umwagiliaji Kata ya Ikweha ambao ulitumia zaidi ya shilingi milioni 800 ulikuwa kama mradi ambao hauna manufaa mpaka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini mradi huu utahuishwa ili lengo lile lililolengwa kujenga uwe na manufaa kwa wananchi wa Ikweha na kata nzima katika kuhakikisha kilimo cha umwagiliaji kinaendelea? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nimshukuru Kaka yangu Kigahe kwa swali lake la msingi, tunatambua changamoto ambayo ameainisha katika Mradi wa Ikweha uliopo katika jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa maelekezo ambayo Mheshimiwa Rais, alitupatia Wizara ya Kilimo, kupitia Tume; moja ni kuhakikisha, vilevile yaani tunahuisha ile miradi ambayo ilitengenezwa zamani lakini bado haina tija kwa wananchi na hiyo ndio kazi mojawapo ambayo Tume wanafanya, ikiwemo kuanzisha maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tu nimthibitishie tu kwamba tuta-*push* kwa haraka sana ili mradi ule uweze kukamilika na kuleta tija ambayo imekusudiwa kwa wananchi, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapunda Mbwilo, swali la nyongeza.

**MHE. BAZILIO K. MBWILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kuishukuru

Serikali kwa kutupatia zaidi ya shilingi bilioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa mifereji ya umwagiliaji Mradi wa Lwafi – Katongolo, ahsante sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha mradi huo ili wakulima waweze kulima zaidi ya mara moja kwa msimu, Serikali inaweza kuwa tayari sasa kutuongeza pesa ili tujenge bwawa la umwagiliaji katika mradi huo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nimthibitishie tu kaka yangu Mheshimiwa Mbwilo, kwa wilaya yako ya Nkasi ambapo kuna majimbo mawili ikiwemo jimbo lako, Mradi huu wa Lwafi – Katongolo baada ya kumalizika kwa skimu, hatua inayofuatia ni kujenga bwawa. Kwa hiyo, ipo katika mipango yetu kwa sababu ni lazima uweke bwawa ili wananchi walime muda wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, skimu zile zinasaidia zaidi wakati wa msimu wa mvua na wakati tunaelekea kumalizika kwa ule msimu wa kilimo. Kwa hiyo, ni sehemu ya mradi wa Serikali kwa hiyo tunachotafuta ni fedha ili ule mradi uanze.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali ya nyongeza yawe mafupi.

Mheshimiwa George Malima, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, katika Jimbo la Mpwapwa kuna ujenzi wa bwawa la umwagiliaji ambao ukikamilika utatumika na kata mbili; Kata ya Chunyu na Kata ya Ng'hambi, lakini ujenzi wake unasuasua ni muda mrefu sasa, lakini halikamiliki.

Je, ni lini Serikali itakamilisha mradi huu ili wananchi wa kata hizi mbili nilizozitaja waweze kuanza kufanya kazi ya kilimo cha umwagiliaji? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nimthibitishie tu Kaka yangu Mheshimiwa Malima, katika eneo la Mpwapwa, katika sehemu ya fedha ambazo tunaendelea kupokea kila mwezi ambazo Hazina imeji-*commit* kutoa kwa Wizara ya Kilimo kwa Tume, shilingi bilioni 25 kila mwezi ni pamoja na kuhakikisha kwamba tunamaliza miradi ya mabwawa na skimu ambazo tayari tumeshazianza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mradi wake upo katika hiyo sehemu na changamoto kubwa ambayo ilikuwa inachelewesha ilikuwa ni utoaji wa zile fedha kwa wakati ule, lakini sasa hivi tunauhakika wa *flow* ya fedha, kwa hiyo, maana yake tutapeleka ili ule mradi ukamilike kama ulivyopangwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asha Baraka, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA R. BARAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante; je, Serikali ina mpango gani kwa *Kibaha DC* kwa ajili ya kilimo cha mboga mboga ambacho ni kilimo cha umwagiliaji ambacho wajasiriamali wengi wanakisubiri kwa hamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kufahamu je, kitaanza lini hicho kilimo cha umwagiliaji wa mboga mboga ambazo mbogamboga hizo zitakuwa zinalisha Mkoa wa Dar es Salaam na mikoa ya jirani? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na napenda tu nimthibitishie dada yangu Mheshimiwa Asha Baraka, kwamba kilimo cha mboga mboga nchini ni moja ya vipaumbele vyetu sisi kama Serikali na niliambie tu Bunge lako Tukufu kwamba sekta ya mboga mboga *(horticulture)* ndio sekta ambayo inakuwa zaidi kuliko sekta nyingine hapa nchini zaidi ya 11% kwa mwaka au kufananisha na sekta nyingine zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo katika moja ya mikakati tuliyonayo ni kujenga ile miradi ya umwagiliaji midogo midogo ambayo siyo mikubwa kama hii ambayo tunatekeleza katika maeneo mengine ya umwagiliaji, ikiwemo kuchimba visima katika hayo maeneo ili yaweze kuwasaidia wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni sehemu ya mpango na ndio maana utaona mpaka sasa hivi tumeshanunua zaidi ya gari 18 kwa ajili ya kuchimba visima katika maeneo kama hayo.

Kwa hiyo, tutafika hapo na tutatekeleza huo mpango ambao nimeueleza ili tuweze kuwasaidia hao wakulima waendelee na kilimo chao, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yannick Ndoinyo, swali la nyongeza.

**MHE. YANNICK I. NDOINYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyofahamu Naibu Waziri, mkataba wa kuanzisha skimu za umwagiliaji katika Kata za Kirangi, Oldonyosambu na Digodigo umesainiwa toka mwezi wa tatu na mkandarasi hajaanza kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba ahadi yako ya kufuatilia changamoto inayomsumbua ili kuiondoa ili akaanze kazi. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kama umemsikia vizuri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Ndoinyo, anachotaka ni ahadi na anafahamu jambo lake na mimi tumekuwa tukilifuatilia pamoja pale ofisini. Nimthibitishie tu kwamba ninalifanyia kazi na tutampa majibu hivi karibuni na hata tukimaliza baada ya Bunge, tunaweza tukaenda wote ofisini kwa ajili ya kujua hatua gani ambayo tumefikia mpaka sasa hivi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Faraji Nandala, swali la nyngeza.

**MHE. FARAJI B. NANDALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili nimweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Ndanda, tumebahatika kupata skimu tatu kubwa za umwagiliaji, lakini skimu hizi utekelezaji wake umekuwa ukisuasua; ile skimu ya Nanganga shilingi bilioni 25, skimu ya Ndanda shilingi bilioni 23 na skimu ya Nanganga kwenye Kijiji cha Maparawe ya shilingi bilioni 25.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni ipi kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba wanapeleka fedha za kutosha ili kuweza kukamilisha utekelezaji wa skimu hizi kubwa tatu za kimkakati na kuleta matumaini makubwa kwa wananchi wa Jimbo la Ndanda? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nimthibitishie tu Mheshimiwa Nandala, Mbunge wa Ndanda kwamba miradi hiyo ni sehemu ya miradi ambayo tumeitengea fedha na tutaendelea kutoa ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kauli ya Serikali ni kwamba tutaleta fedha kwa sababu tunauhakika wa kupata fedha sasa hivi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Mbulu Vijijini kuna mabwawa mawili; Bwawa la Dongobesh na Bwawa la Mangisa, ambalo linahudumia Skimu ya Dongobesh lakini pia Skimu ya Kata ya Yaeda Ampa na Bashay. Je, Serikali inampango gani wa

kuboresha mabwawa haya kwa kuwa yamejaa matope na mengine yamebomoka? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nimthibitishie tu Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas, Mbunge wa Mbulu Vijijini kwamba bahati nzuri kwenye maeneo hayo ya Dongobesh, nimefika mimi mwenyewe na ni sehemu ya miradi ambayo sisi kama Serikali tunaitekeleza na miongoni mwa mikakati yetu tukishamaliza ujenzi wa skimu basi na yale mabwawa yote yatakamilika kwa wakati. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mariki, swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji ya Mwamkulu, umekuwa ukisuasua kutokana na ucheleweshwaji wa malipo kwa mkandarasi, hali inayopelekea skimu hii kutokamilika kwa wakati. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha ili kukamilisha ujenzi wa skimu hii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, labda nijibu swali hili kwa ujumla kwamba moja; kwa sasa hivi Wizara ya Kilimo kupitia Tume, tunatekeleza zaidi ya miradi 780 na miradi yote hii inahitaji fedha na *flow* ya fedha kila mwezi tumekuwa walau tukipokea kati ya shilingi bilioni 10 mpaka shilingi bilioni 25. Kwa hiyo, tunakuwa tunapeleka kwa mgawanyo ili kuhakikisha miradi yote inakwenda sambamba, hata mradi ambao ameeleza Mheshimiwa Martha Mariki, ni sehemu ya miradi ambayo tunaitekeleza.

Kwa hiyo, niwathibitishie tu Waheshimiwa Wabunge, miradi itakamilika kama ilivyopangwa, kwa sababu tuna uhakika wa kupeleka fedha ambazo Serikali imekuwa ikitupatia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ado Shaibu Ado, swali la nyongeza.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kuniona. Katika jimbo langu la Tunduru Kaskazini, kuna Mradi wa Umwagiliaji wa Nambalapi (Skimu ya Nambalapi) ambao bado unasuasua kwa sababu ya uwezeshaji wa kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kujua kauli ya Serikali ni lini mradi ule utakamilika? ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru ndugu yangu Ado Shaibu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini. Moja, tutaleta fedha kuhakikisha Mradi wa Nambalapi unakamilika kama ilivyopangwa, lakini huwa tunazingatia, kunakuwa na *variation* ambazo kimkataba tunakuwa tumeziweka, lakini lengo la Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha miradi hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tuta-*push* ikamilike kama ilivyopangwa ama isiende mbali na ule muda ambao tumepanga ili kuhakikisha kwamba inawanufaisha wananchi ambao wanahitaji matumizi ya zile skimu, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Enock Zadock Koola, Mbunge wa Vunjo, sasa aulize swali lake.

Na. 533

**Ujenzi wa Soko Kubwa la Mazao Lokolova-Vunjo**

**MHE. ENOCK Z. KOOLA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga soko kubwa la kimataifa la mazao katika eneo la Lokolova ili kunufaika na ukaribu wa mpaka wa Kenya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Serikali inatambua umuhimu wa kujenga masoko ya kimkakati ya kimataifa ya mazao katika maeneo ya mipakani ikiwemo Lokolova ili kunufaika na fursa ya biashara ya kuvuka mipaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo inaendelea kufanya tathmini ya maeneo yenye kipaumbele kulingana na vigezo vya uzalishaji wa mazao, wingi wa biashara ya mpakani, pamoja na upatikanaji wa rasilimali na mahitaji ya miundombinu likiwemo eneo la Lokolova. Ujenzi wa soko hilo utatekelezwa baada ya kukamilika maandalizi ya kitaalamu ya mradi husika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Enock Zadock Koola, swali la nyongeza.

**MHE. ENOCK Z. KOOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza nishukuru majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutambua umuhimu wa soko hili kubwa la Lokolova, lakini majibu haya yamekuwa ya jumla jumla. Sasa naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa moja ya changamoto imekuwa upatikanaji wa hati ya hili shamba ambalo halmashauri ya Wilaya ya Moshi ilikuwa imeahidiwa ekari 140, je, Serikali ina kauli gani kwa Mrajisi

wa Vyama vya Ushirika kuharakisha zoezi hilo la utoaji wa hati ili kazi ianze? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je Serikali inaweza kutoa kauli gani mbele ya Bunge hili Tukufu ya kwamba lini hati itatolewa na lini mradi huu wa soko hili la kimataifa Lokolova utaanza? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Enock Koola, Mbunge wa Vunjo na bahati nzuri anafahamu suala hili hata wakati tukiwa na ziara na Mheshimiwa Waziri Mkuu tulishalitolea tamko na Mheshimiwa Waziri Mkuu alituelekeza kwamba tuhakikishe eneo lile linajengwa soko, lakini miongoni mwa changamoto ndogo iliyokuwa imejitokeza ni pamoja na hati ya eneo hilo kuwa chini ya mrajisi na Mrajisi vilevile wa vyama yupo chini ya Wizara ya kilimo. Kwa hiyo kuna hatua ambazo lazima zifuatwe ndiyo maana tukaeleza hapa kwamba kuna mambo ya kitaalam kidogo yakishapata kukamilika ikiwemo kukabidhi hati baada ya majadiliano ya pande zote mbili, basi sisi kama Wizara tutajenga soko hilo katika eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimwambie tu kwamba tunaendelea na hizo taratibu naamini zitaisha kwa wakati mwafaka na zikishakamilika basi sisi tutaanza mradi wa ujenzi wa soko katika eneo hilo. Hayo ndiyo majibu ambayo ninaweza nikampatia kwa wakati huu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Edifonsi Joackim Kanoni, swali la nyongeza.

**MHE. EDIFONSI J. KANONI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza. Kwanza niipongeze Serikali kwa kuendelea kuweka ruzuku katika pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 90 ya wakazi na wananchi wa jimbo la Kalambo ni wakulima, mwaka huu tunatarajia kuvuna tani laki tatu za mahindi, lakini hali ya soko ni mbaya sana. Nini mpango wa Serikali kuhakikisha wanakuwa na soko la uhakika ili kunusuru wananchi hawa ambao wamekopa mikopo mbalimbali katika taasisi zetu za benki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, natambua kazi nzuri anayofanya Mheshimiwa Kanoni, Mbunge wa Kalambo katika jimbo lake na nimthibitishie tu kwamba ni kweli mwaka huu tunamatarajio makubwa sana hususani kwa wakulima wa mahindi. Nyanda za Juu Kusini nafikiri tutavuna zaidi kuliko kipindi kingine chochote. Sasa changamoto kubwa imekuwa ni soko na soko letu la kwanza ni kupitia *NFRA* ambao ndiyo wamekuwa wanunuzi wakubwa wa mahindi hapa nchini, lakini kutokana na mahitaji makubwa ndiyo maana mwaka huu *NFRA* wamefungua masoko matano katika nchi ambazo zinatuzunguka, yaani ikiwemo sasa tunakwenda Congo, Zambia, Malawi, Kenya, Uganda pamoja mpaka na Rwanda. Ni maeneo ambayo tumeyafungua masoko ili kuongeza wigo wa wananchi kuuza mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, moja ya mpango wa kujenga masoko yale ya kimkakati katika maeneo yanayozalisha mazao mengi, eneo la jimbo la Kalambo ni sehemu hiyo ili tuweze kurahisisha ufanyaji wa biashara ya mazao hayo.

Kwa hiyo, hicho ndicho ninachoweza kumweleza Mheshimiwa Mbunge ambacho ni sehemu ya mikakati ya Serikali tuliyonayo kwa mwaka huu, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kafiti Kafiti, swali la nyongeza.

**MHE. KAFITI W. KATIFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi hii kuuliza swali la nyongeza kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ilemela.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua, je, Serikali ina mpango wowote wa kuzielekeza halmashauri kutenga maeneo kwa ajili ya skimu za umwagiliaji ili vijana waweze kujiajiri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nimshukuru kaka yangu Kafiti, Mbunge wa Ilemela kwa kulikumbusha hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali tumeshatoa maelekezo kwa halmashauri zote nchini, moja kutenga maeneo kwa ajili ya umwagiliaji, lakini vilevile kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za *BBT* ambapo shughuli hizo Wizara ndiyo itakayozihudumia na wanufaika watakuwa katika maeneo hayo. Kwa hiyo, ni maelekezo ambayo Serikali tulishayatoa na nitumie nafasi hii vilevile kuwakumbusha wakurugenzi kutenga maeneo hayo ili sasa Serikali tuingize katika mpango kwa ajili ya utekelezaji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joshua Nassari, swali la nyongeza.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona na mimi nitumie fursa hii kwanza kabisa kuipongeza Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Naibu Waziri hapa kwa namna ambavyo mmeendelea kutuwezesha sisi wakulima wa kule kwetu Meru kwenye masuala mazima ya mbolea ya ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kule kwetu Meru kuna maeneo mengi sana na Mheshimiwa Naibu Waziri anayafahamu, watu wa Meru walikwishapata umoja wa UWAWAME ambao walishawahi kukuualika hata wewe Mheshimiwa Naibu Waziri Umoja ya Wakulima na Wafugaji kule kwetu, lakini watu wetu wanalima sana karoti na viazi kwenye vijiji vingi ambavyo kwa sehemu kubwa vinakwenda nje ya nchi, lakini hawa wachuuzi wanafata shambani moja kwa moja hatuna soko la kisasa pale Meru na unajua hivho kilimo ni kikubwa sana kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba tu kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kama yuko tayari tuambatane mimi na yeyeakapite akaone hicho kilimo kinachofanyika ili tuangalie ni kwa namna gani tunaweza basi tukajadiliana na halmashauri na tukatengeneza soko la kimataifa la karoti na viazi pale Meru? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nimshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Joshua Nassari, Mbunge wa Arumeru Mashariki kwa swali lake la msingi. Nimthibitishie tu kwamba Arumeru naiifahamu vizuri na niko tayari kurudi tena na tena kufanya hiyo kazi na bahati nzuri Bunge limebakiza wiki mbili mpaka tatu kuisha, kwa hiyo baada ya Bunge nitafika maeneo yote kwa sababu hiyo kazi mimi naweza. Kwa hiyo tutakwenda kwa ajili ya kujionea hizo kazi.  Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saasisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza nashukuru sana Wizara ya Kilimo, Waziri na Naibu Waziri kwa namna ambavyo wametuletea fedha za kujenga soko la Mula, lakini soko lile linaendelea na ujenzi vizuri ila ni dogo ukilinganisha na idadi ya wafanyabiashara walioko soko la Tolu ambalo soko lile la Tolu sasa hivi ni hatarishi watu wanagongwa pale.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutuongezea fedha kwa sababu tayari tumetenga eneo lingine pale linapojengwa soko la Mula liongezwe soko lingine na wale wa Tolu wahamie pale Mula?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nimshukuru kaka yangu Mheshimiwa Saashisha Mafuwe Mbunge wa Hai. Nafahamu jitihada zako kwa wananchi wako,

kwa hiyo tutatuma tume iende pale ifanye tathmini kwa ajili ya hayo mahitaji baada ya hapo tuanze taratibu za kitaalam ili tufanye *expansion* katika eneo lako. Kwa hiyo, tuwathibitishie wananchi kwamba Serikali tunakuja hapo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Asha Juma Kombo, Mbunge wa Mfenesini, sasa uliza swali lake.

Na. 534

**Mkakati wa Serikali Kuhakikisha Ajira kwa Wahitimu wa *VETA***

**MHE. ASHA JUMA KOMBO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wahitimu wa Vyuo vya *VETA* nchini wanapata ajira au fursa za kujiajiri baada ya kumaliza mafunzo yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Elimu Mheshimiwa Wanu Hafidh, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na kwa ruhusa yako naomba nijibu swali namba 534 la Mheshimiwa Asha Juma Kombo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha wahitimu wa Vyuo vya *VETA* wanapata ajira au fursa za kujiajiri baada ya kuhitimu mafunzo yao. Miongoni mwa mikakati hiyo ni utekelezaji wa Mpango wa Ushirikiano kati ya Taasisi za Elimu na Mafunzo, Waajiri na Viwanda uliozinduliwa tarehe 9 Februari, 2026 na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, wenye lengo kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi za

elimu na mafunzo kwa upande mmoja na waajiri pamoja na viwanda kwa upande mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha mafunzo yanayotolewa yanazingatia mahitaji halisi ya soko la ajira, kupitia mkakati huo wahitimu watapata umahiri unaohitajika na waajiri, uzoefu wa vitendo pamoja na fursa za kuunganishwa na waajiri. Aidha, Serikali inaendelea na zoezi la utambuzi wa mahitaji ya ujuzi *(skills mapping)* katika ngazi zote za elimu na mafunzo ya ufundi nchini linalotarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2026 ambapo litasaidia kubaini mahitaji ya ujuzi yaliyopo na yanayotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, matokeo yake yatawezesha utoaji wa mafunzo yanayoendana na mahitaji ya soko la ajira. Vilevile Serikali inaendelea kuimarisha mafunzo ya ujasiriamali kwa wanafunzi wa *VETA* ili kuwajengea uwezo wa kuanzisha na kuendesha shughuli zao za kiuchumi baada ya kuhitimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asha Juma Kombo, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA JUMA KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali madogo mawili.

Swali la kwanza, kwa kuwa halmashauri, miji na manispaa zinatoa mikopo kwa makundi ya vijana, wanawake na wenye ulemavu, je ni kwa kiasi gani wahitimu wa *VETA* wanazingatiwa katika utoaji huo wa mikopo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kumekuwa na ukosefu wa maeneo ya kufanyia shughuli kwa wahitimu wa *VETA*, je, Serikali ina mkakati gani wa kutenga maeneo maalum kwa wahitimu wa *VETA* kujifanyia shughuli zao za kujiajiri? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asha Juma Kombo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia mamlaka za Serikali za mitaa ni kweli inatoa mikopo kwa ajili ya makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kwa mujibu wa sheria, kanuni na mwongozo uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wahitimu wa *VETA* wanaokidhi sifa wanahaki ya kuomba mikopo hii kama wananchi wengine na mara nyingi wanazingatiwa wakiomba kwa sababu ujuzi wao unawawezesha kuwaongezea uwezo wa kuandaa miradi yenye tija. Kwa hiyo, mikopo hii haibagui kijana yeyote hadi wale ambao wanatoka Vyuo vya *VETA* wanaruhusiwa kuomba mikopo hii na kupata nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kwamba wahitimu wa *VETA* wanaendelea kuomba mikopo hii na huwa kuna ongezeko la wahitimu hawa kila mwaka. Kwa hiyo, pamoja na kwamba *turn up* ni nzuri tunaendelea kuhamasisha wanafunzi wa wahitimu wa *VETA* kuendelea ku-*access* fursa hizi na kuhakikisha kwamba wanapata mikopo hii kama vijana wengine waliopo mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, Serikali inatambua changamoto ya upatikanaji wa maeneo ya kufanya shughuli za kujiajiri kwa wahitimu wa vyuo mbalimbali ikiwemo *VETA*. Serikali inaendelea kutenga maeneo maalum kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa, inaendelea kutenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za uzalishaji biashara, viwanda vidogo na karakana katika mipango ya matumizi bora ya ardhi na mipango miji.

Kwa hiyo, pamoja na kwamba tunatambua kuna maeneo machache, lakini Serikali imeendelea kutenga maeneo haya ili kuwawezesha wahitimu kupata maeneo na sehemu za kujiajiri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salma Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, awali ya yote naomba niipongeze Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutoa ajira kwa walimu na taasisi nyingine, hongera sana. Sambamba na hilo niwapongeze walimu kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya na hata wale walimu ambao wanajitolea kufanya hizo kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, nini kauli ya Serikali kwa walimu wale ambao wanajitolea angalau kupata kitu kidogo dogo yaani *incentive* ili na wao waweze kukidhi mahitaji yao? Nasema haya kwa sababu nina mfano hai katika jimbo langu la Mchinga walimu wanajitolea, lakini hawana kitu chochote wanachopata kutoka Serikalini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mama Salma Kikwete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze kwa kuwasemea walimu wenzake, lakini katika swali hili nadhani Mheshimiwa Waziri Mkuu alishalitolea maelekezo kwamba halmashauri ziendelee kutenga fedha kwa ajili ya walimu wanaojitolea katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo na mimi nasimama na msimamo wa Waziri Mkuu kwamba halmashauri ziendelee kutenga fedha na alitoa maelekezo kwamba hakuna kiwango maalum ambacho kimekuwa *fixed* kwa ajili ya walimu hawa, lakini halmashauri zilipe kwa mujibu wa uwezo wao kuona kwamba walimu wanaojitolea nao angalau wanapata chochote.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Phillipo Mulugo, swali la nyongeza.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kuna ujenzi unaendelea wa Chuo cha *VETA* pale Wilaya ya Songwe takribani mwaka huu ni mwaka wa nne na ujenzi

unasuasua mpaka sasa hakuna kinachoendelea. Naomba kauli ya Serikali, lini ujenzi wa *VETA* utamalizika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mulugo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Mkoa wa Songwe ambao unaendelea na asilimia ya ujenzi ule umeshafika mahala pazuri sana. Nadhani tushakubaliana hapa kwamba fedha tayari zimeshatoka na fedha zimeanza kuingia katika vyuo ambavyo vinaendelea kujengwa na *by September,* 2026 tunatarajia kwamba vyuo hivi vyote vitakuwa vimemalizika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, sasa uliza swali lake.

Na. 535

**Ujenzi wa Barabara ya Bombo Mtoni - Mkomazi**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Bombo Mtoni - Umba hadi Mkomazi ambayo ipo kwenye Ilani ya CCM utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa *Engineer* Kasekenya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Bombo Mtoni - Umba – Mnazi Langoni – Mkomazi ni muunganiko wa Barabara za Bombo Mtoni – *Umba Junction* na ile ya *Umba Junction* – *Mkomazi Junction* zenye urefu wa kilometa 128.57 zinazohudumiwa na *TANROADS* Mkoa wa Tanga. Serikali inaendelea na taratibu za ununuzi wa mhandisi mshauri kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi ya kuijenga kwa kiwango cha lami. Baada ya usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii imekuwa ni kiungo muhimu cha kukuza uchumi wa utalii kati ya Hifadhi ya Saadani na Hifadhi ya Mkomazi, lakini pia inasaidia sana kuboresha usafiri kwa sababu sasa hivi Bandari ya Tanga inafanya kazi vizuri, lakini Barabara ya Tanga – Segera - Korogwe hadi Arusha imezidiwa sana na barabara hii ndiyo inaweza ikaja kuwa mbadala wa Barabara ya Tanga - Korogwe hadi Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuharakisha mchakato huu ili barabara hii ianze kujengwa kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, barabara ya kutoka Lushoto kwenda Lukozi - Manolo - Mkelei - Sunga hadi Mtae bado haijafanyiwa usanifu, je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuifanyia

usanifu wa kina barabara hii ili fedha zitakapopatikana na yenyewe iweze kujengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi Mbunge wa Mlalo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara aliyoitaja ni muhimu sana na ni kweli kwamba itakuwa na manufaa sana ikijengwa kwa kiwango cha lami, ikiwa ni kukuza utalii kwa ile mbuga ya Mkomazi, lakini pia itapunguza msongamano kwenye barabara hii kuu ya Korogwe kwenda Moshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana tunapoongea sasa hivi tumesema tuko kwenye hatua za mwisho na barabara hii inasimamiwa na makao makuu *TANROADS* kwa ajili ya kuisimamia kufanya usanifu kwa sababu ya umuhimu wake, lakini pia inaunganisha hiyo Mikoa ya Tanga na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hatutaruka hatua, lakini tutahakikisha kwamba tunasimamia kwa uharaka ili tukamilishe hicho kitendo cha kuisanifu, halafu tuanze kutafuta fedha kwa ajili ya kuijenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kuhusu swali lake la pili, ni kweli kwamba kipande cha Lukozi kwenda Mtae ni sehemu ya barabara ya kutoka Lushoto – Magamba – Lukozi - Mnalo kwenda *Umba Junction* ambapo atakubaliana na mimi kuwa wakati tupo kwenye ziara na Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo tuweze kufanyia usanifu, lakini ikiwa ni Lukozi - Mlalo kwenda *Umba Junction* ambapo tayari tumeshakamilisha na mkandarasi tumeshampata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipande ambacho amekisema cha Lukozi kwenda Mtae tutaendelea kukifanyia ukarabati lakini nimhakikishie kwamba kwa kuwa ni kipande kifupi,

tutaangalia uwezekano kama mkandarasi ambaye *I mean* mhandisi mshauri ambaye tayari ameshawekewa hiyo kazi kwa sababu ni kipande kifupi sana cha Lukozi kwenda Mtae, tuone kama tutaweza kumpa *addendum* ili aweze pia kufanya usanifu wa hicho kipande. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge naona kwenye orodha mpo wengi, naomba maswali yawe mafupi.

Mheshimiwa Aysharose Mattembe, swali la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa barabara inayoanzia Ibugunoshamba, inakwenda Kinyangiri - Gumanga, ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa Mkoa wa Singida na Simiyu. Sasa ningependa kujua ni lini Serikali itapeleka fedha ili kuanza kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, barabara hii ilikuwa imeshatengewa fedha na tuliitangaza, tukapata mkandarasi, lakini mkandarasi huyu tulishindwa kukubaliana naye kwa sababu ya gharama. Kwa hiyo, barabara hiyo, inatangazwa tena ili iweze kujengwa ikiwa ni kuunganisha kwa kweli barabara ya kuu na makao makuu ya wilaya, lakini ndiyo kwenda huko Sibiti kwenda Bariadi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naomy Mwaipopo, swali la nyongeza.

**MHE. NAOMY D. MWAIPOPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Jimbo la Kigoma Mjini kuna barabara inatoka Katosho - Kibirizi mpaka Bandari ya Kibirizi,

na barabara hii ni ya muhimu sana kwa uchumi wa Kigoma. Tuliomba kwamba barabara hii itoke kwenye Wizara ya TAMISEMI ihamishiwe Wizara ya Ujenzi.

Je, mpaka sasa ni hatua gani imefikiwa kubadilisha barabara hii kutoka TAMISEMI kwenda Ujenzi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ni kweli kwamba kuna taratibu za kupandisha barabara kutoka *TARURA* kuja *TANROADS* ambapo lazima kikao cha Mfuko wa Barabara kikae, lakini pia *RCC* iweze kukaa na kupitisha hizo barabara na kuzileta Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue hili suala, niweze kuona kama hizo taratibu zimeshafika na hiyo barabara iko ofisini kwetu kwa sababu mwenye mamlaka ya kupandisha barabara hadhi ni Waziri mwenye dhamana ya Ujenzi, hasa baada ya kupeleka timu kujiridhisha kwamba hiyo barabara ina sifa hizo.

Kwa hiyo, naomba nilichukue niweze kufuatilia kama limeshafika ofisini kwetu na wataalamu wameweza kwenda na nione nini wameshauri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Patali Patali, swali la nyongeza.

**MHE. PATALI S. PATALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Barabara ya Mbalizi - Shigamba ni moja ya barabara muhimu sana na ya kimkakati Jimbo la Mbeya Vijijini. Nichukue fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini kuishukuru sana Serikali kwa sababu imeji-*commit* kuanza ujenzi wa kilometa 10 wa barabara hii. Kwetu hili ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa hizi kilometa 10 ambazo Serikali imeji-*commit*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ni kweli tulitenga kilometa 10 na hii barabara taarifa zote zimeshakamilika, kinachosubiriwa ni kibali cha kuisaini hiyo barabara ili hizo kilometa kumi zianze kujengwa. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nina uhakika katika kipindi cha bajeti, *I mean* baada ya kumaliza kipindi hiki cha mwaka wa fedha, hiyo barabara itaenda kuanza hizo kilometa kumi kama tulivyoahidi kwa sababu taratibu zote ziko tayari, kinachosubiriwa tu ni kusaini huo mkataba. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mkwamo mkubwa sana unaotokea katika Barabara ya Kitonga, magari makubwa kukwama ya uchumi pamoja na wananchi wanaoishi katika kata zile tatu wanapokwenda hospitali, Serikali ilitoa ahadi ya kujenga njia nne.

Je, ni lini sasa utekelezaji utaanza kwa sababu changamoto hiyo ni kubwa mno, mno, mno? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Ritta Kabati, Mbunge wa Kilolo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitonga ni barabara kuu *T1* ambayo hata katika bajeti imepewa umuhimu wake kwamba tunakwenda kuanza kujenga njia nne kuanzia pale chini na tutaanza na kilometa nne kujenga njia nne ili kupunguza msongamano, lakini pia inapotokea changamoto tusiweze kuzuia kabisa hiyo njia.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge hata kama utapita kwenye vitabu vyetu vya bajeti tumeipa kama ni miradi ya kipaumbele katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka ambao mmetupitishia. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara hii hii, Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 536

**Ujenzi wa Barabara ya Mbalizi – Mkwajuni**

**MHE. JULIANA D. SHONZA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza rasmi ujenzi wa Barabara ya Mbalizi hadi Mkwajuni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Mbalizi – Mkwajuni yenye urefu wa kilometa 92 ni sehemu ya barabara ya mkoa ya Mbalizi – Chang'ombe – Galula – Mkwajuni – Saza – Patamela hadi Makongolosi yenye urefu wa kilometa 117 inayounganisha Mikoa ya Mbeya na Songwe. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mkoa wa Mbeya, mkandarasi anaendelea na matengenezo makubwa ya kilometa 3.5 za lami kuanzia Mji Mdogo wa Mbalizi katika Kijiji cha Utengule kuelekea Mkwajuni. Aidha, kwa Mkoa wa Songwe mkandarasi anaendelea na maandalizi ya vifaa vya ujenzi ikiwemo mitambo

kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kipande chenye urefu wa kilometa tano kuanzia Mkwajuni kuelekea Saza. Kwa sehemu zilizobaki, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, swali la nyongeza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwenye majibu ya msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba mkandarasi yupo kwenye maandalizi ya vifaa, lakini uhalisia uliopo *site*, changamoto kubwa ambayo inapelekea barabara hii ya Mbalizi mpaka Mkwajuni kutokukamilika hususan upande wa barabara ya Wilaya ya Songwe, changamoto kubwa ni fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hili kwa sababu si Barabara tu ya Mbalizi mpaka Mkwajuni, lakini pia Barabara ya Mlowo - Kamsamba ambayo mpaka sasa hivi tunavyoongea hakuna kinachoendelea pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niulize swali langu la nyongeza, Mheshimiwa Naibu Waziri; je, Serikali sasa haioni kwamba kuna umuhimu mkubwa wa kuongeza fedha kwenye bajeti? Kwa sababu fedha ambayo Serikali imetenga kwenye bajeti hii ni ndogo sana na ni wazi tukienda kwa mwenendo wa kutenga fedha hivi kidogo kidogo, barabara hizi mbili zitachukua miaka mingi sana kuweza kukamilika. Mheshimiwa Naibu Waziri, unatoka ndani ya Mkoa wa Songwe, unajua changamoto ambazo wananchi wanapata, naomba utujibu, je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza fedha ya kutosha ili barabara hizi ziweze kukamilika kwa wakati? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza kwa kufuatilia ujenzi wa miundombinu katika Mkoa wa Songwe na barabara aliyouliza sambamba na Barabara ya Mlowo -

Kamsamba ni barabara ambazo zinatekelezwa na mkandarasi mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulishatangaza na tulishampata mkandarasi, lakini changamoto ni kwamba hakupata malipo ya awali ambayo tumeahidi kwamba sasa miradi yote iliyokuwa imesimama tunakwenda kuikwamua ikiwa ni pamoja na huyu mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuongeza fedha, ni kwamba tunaposema tunajenga kwa awamu, kwa hiyo, tukishakamilisha hizo kilometa tano kadri fedha itakavyopatikana, lengo la Serikali ni kukamilisha barabara yote hiyo kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nauliza kuhusu Barabara ya Makete – Mbeya; tunafahamu kwamba mkandarasi amelipwa. Nilikuuliza hapa kwamba lini ataenda, hajaenda hadi leo, licha ya kwamba ulitoa tamko, lakini Wana-Makete wamekuwa njia panda kuhusu barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imetoa fedha kwa zile *certificate* ambazo amezi-*rise* mkandarasi, lakini hadi sasa hivi hajafika, na mimi nimekuona wewe, nimemuona Waziri na wataalamu wako wa *TANROADS* kwa nyakati tofauti kuwaomba kuhusu barabara hii.

Je, hauoni ni wakati sahihi wa kuunda kikosi maalum kikafanye tathmini, nini kinaendelea dhidi ya mkandarasi huyu? *Either* uwezo ni uko chini au kuna changamoto nyingine ambayo inaendelea? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Festo Sanga, Mbunge wa Makete kwamba Serikali inafuatilia kwa ukaribu sana na hasa

kulingana na jitihada ambazo mara kwa mara umekuwa ukitukumbusha, si ofisini na hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulichofanya kwanza baada ya kukutana na uongozi wa huyo mkandarasi, sasa hivi Waziri ameagiza kati ya tarehe 12 na 15 *management* ya mkandarasi huyo kutoka China waje wakutane ili tuchunguze tatizo ni nini, ili ikiwezekana Serikali iweze kuanza kuchukua hatua za kimkataba, kwa nini baada ya kulipwa bado ameshindwa kuanza kazi?

Kwa hiyo, tunalifuatilia na tutaendelea kutoa majibu kwamba wakandarasi kama hao, kama itaonekana ameshindwa kazi basi ziko taratibu za kimkataba ambazo tutazichukua. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Samira Amour, swali la nyongeza.

**MHE. SAMIRA K. AMOUR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi kwa kiwango cha lami Barabara ya Lusaunga - Rusumo Mkoani Kagera ili kukuza biashara kati ya Tanzania na nchi jirani? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba wakati Mbunge anauliza swali tupunguze makofi ili Waziri aweze kusikia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ujenzi wa Barabara ya Lusaunga - Rusumo ni ukarabati mkubwa ambao unafanywa tukisaidiana na wenzetu wa *World Bank.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkandarasi ambaye yuko *site* mpaka sasa hivi yuko ndani ya muda wa kazi, labda kama Mheshimiwa Mbunge ameona kuna changamoto yoyote basi tuko tayari kuifuatilia, lakini amekuwa akilipwa kwa muda na amekuwa akifanya kazi hiyo na tunauhakika ndani ya muda ambao amepangiwa kimkataba, atakamilisha hiyo kazi ambayo kwa kweli tunaamini baada ya kufanya hivyo wenzetu

wanaofanya biashara kati yetu na Wanyarwanda kwa kweli watakuwa sasa wamepata barabara nzuri sana ambayo kimsingi barabara hii ilikuwa imekufa kabisa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itakamilisha kujenga kwa kiwango cha lami maeneo korofi katika Barabara ya kwa Mbuyu wa Mjerumani - Mbulu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, tumeendelea kujenga kwa kiwango cha zege ama lami katika maeneo korofi. Na tumeshakamilisha usanifu lakini wakati tunaendelea kujenga hayo maeneo korofi, Serikali pia inaendelea kutafuta fedha ili iweze kuijenga barabara yote hiyo kwa kiwango cha lami.

Kwa hiyo, kadri fedha inavyopatikana tutaendelea kukarabati yale maeneo korofi hasa katika ile miinuko kati ya Mbuyu wa Mjerumani na Mbulu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abubakar Omari, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKAR A. OMARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa fursa hii. Mimi ningependa kuuliza; kuna Barabara kutoka Choma kwenda Chibiso na Chibiso kwenda Samuye, Mkoa wa Shinyanga. Tuliomba toka mwaka 2024 ipandishwe daraja ya kuwa barabara ya *TANROADS*, ukizingatia kwamba barabara kuu ya kutoka Puge - Ziba hadi Choma iko kwenye upembuzi yakinifu na inakaribia kufikia 80%.

Je, ni lini barua hii itajibiwa ambayo ilishafika ofisini kwa Waziri toka mwaka 2024? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijamsikia vizuri pale mwanzoni swali lake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abubakar taja barabara hiyo.

**MHE. ABUBAKAR A. OMARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kuna kipande cha barabara kutoka Choma kwenda Chibiso, kilometa 15 Mkoa wa Tabora, kiliombewa kupandishwa daraja kwenda kwa *TANROADS*. Na kipande kingine cha kutoka Chibiso kwenda Samuye, Mkoa wa Shinyanga. Barabara hiyo ilishaombewa kupandishwa daraja toka mwaka 2024 mpaka leo hii barua hii haijapata majibu. Je, Serikali imefikia wapi suala hili? Naomba majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani umelipata vizuri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kama nilivyosema kwenye swali moja la kupandisha hadhi, barabara kama hazipo *TARURA* bado nakuwa siwezi kuzielewa, lakini nimuombe Mheshimiwa Mbunge kama iliombewa, kuna barabara zinaweza zikaombewa zikawa na sifa ya kupandishwa ama zikashindwa kupata sifa za kupandishwa kuja *TANROADS*.

Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge pia kwamba ni suala rahisi, twende pale Wizarani baada ya hapa tuone kama mkoa ulishaleta hayo maombi na mapendekezo ama nini timu iliyokwenda ilishauri *and then* nadhani tutakuwa kwenye hali nzuri ya kuelewa Serikali ilisema nini kuhusu hivyo vipande viwili vya barabara kupanda hadhi kutoka *TARURA* kwenda *TANROADS*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza niendelee tu kusisitiza kwamba zile Barabara za

Mlowo - Kamsamba na Barabara ya Mbalizi - Songwe wajitahidi watupatie fedha kwa sababu ni barabara za muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na swali langu la msingi kwenye eneo la wakandarasi wa Barabara ya Ruanda - Iyula mpaka Ileje; ni kwa nini wakandarasi hawa hawapatiwi fedha kiasi kwamba inapelekea wanashindwa kufanya kazi kwa ufanisi na kuwalipa watumishi wao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ametaja barabara kama tatu, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba moja ya changamoto ambayo tumeisema hata wakati tunawasilisha Bunge, ni kwamba barabara nyingi zilikuwa zimesimama kwa sababu ama tulishindwa kuwalipa hati za malipo ama tulishindwa kuwalipa kwa wakati malipo ya awali na tuliahidi na tunaendelea kuahidi kwamba sasa miradi yote hiyo ambayo wakandarasi ama walikuwa wanasuasua kwa kukosa fedha, sasa tunakwenda kukwamua hiyo miradi yote ikiwemo hiyo Barabara ya Ruanda - Idiwili ambayo inajengwa na wakandarasi wa kike, lakini kwenda kuanza Mradi wa Mlowo - Kamsamba na huo ambao barabara aliuliza Mheshimiwa Mbunge ya kutoka Mbalizi kwenda Mkwajuni kilometa hizo tano. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendela na swali linalofuata, Mheshimiwa *Engineer* Johnston Johansen Mutasingwa, Mbunge wa Bukoba Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 537

**Ujenzi wa Barabara ya Rwamishenye**

**MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara ya njia nne katika Barabara ya Rwamishenye – Kastamu yenye urefu wa kilometa moja?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Rwamishenye – Kastamu yenye urefu wa kilometa moja ni sehemu ya barabara kuu ya Bukoba (Rwamishenye) – *Bukoba Port (Custom)* yenye urefu wa kilometa 4.6 inahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* Mkoa wa Kagera. Ujenzi wa barabara hii ulianza katika sehemu ya Mitaga – Rwamisenye (kilometa moja), ambapo utekelezaji unaendelea na umefikia 85%. Aidha, mradi huu unategemea kukamilika tarehe 30 Juni, 2026. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Johnston Johansen Mutasingwa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza napenda niishukuru Serikali kwa majibu mazuri iliyoyatoa. Vilevile, nitoe shukrani kwa kazi kubwa na njema inayofanyika katika barabara hiyo maana naona ujenzi wake unaendelea vizuri. Mkandarasi akilipwa pesa kidogo anayodai nahisi hiyo kazi itaweza kumalizika kwa muda uliosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza; je, katika barabara hiyo hiyo, Serikali itaanza lini ujenzi wa Daraja la Kasarani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; katika kipande hicho hicho Serikali imeshafanya *feasibility studies* kuanzia *Rwamishenye roundabout* kwenda Kyaka-Ilabwa, na kutoka *Rwamishenye roundabout* kwenda Ibura. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa njia nne katika maeneo hayo ambayo *feasibility studies* imeshakamilika? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nimshukuru Mheshimiwa Mhandisi Johnston Johansen Mutasingwa kwanza kwa kutambua jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita

katika kubadilisha na kuboresha Mji wa Bukoba kwa kujenga barabara za njia nne. Hii ndiyo kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya, si katika Mkoa wa Kagera tu au Mji wa Bukoba, lakini katika miji mingine, lakini pia nimshukuru na kumpongeza kwa kufuatilia uboreshaji wa barabara zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu daraja hili alilolitaja la Kasarani, lipo kwenye barabara hii ambayo tunaijenga kwa awamu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Bukoba kwamba hili daraja kwa sasa limeonekana mvua ikinyesha maji yanapita juu. Kwa hiyo, tunakwenda kulibadilisha hilo daraja, tutalijenga daraja upya, lakini kama tulivyosema, kwa awamu. Kwa hiyo, awamu ya kulijenga daraja, tutalijenga daraja jipya kabisa tofauti na hilo ambalo lipo. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuendelea kujenga njia nne kwenye barabara aliyoitaja ambayo ni *main road* kuelekea Kyaka, lakini na kuja njia ya Dar es Salaam. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba usanifu uko kwenye hatua za mwisho kabisa. Mara baada ya kukamilika tutaijenga hiyo barabara kwa njia nne, kwa sababu imekuwa ndiyo sasa inaweza ikasaidia kupunguza misongamano, lakini pia na mikwamo ya barabara katika miji yetu ambayo sasa hivi biashara zimetanuka na miji imekuwa na magari mengi sana. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunafanya usanifu, lengo ni kujenga njia nne kwa kiwango cha lami, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, Barabara ya Sanzati – Nata imekuwa kama vile hame au jambo lingine limekuwa kubwa sana. Sasa mimi sielewi, ni mkakati gani wa Wizara uliopo wa kumalizia ile barabara au tuseme kwamba hiyo barabara Serikali imeiacha tutangazie wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ni kweli barabara hii imechukua muda, lakini imechukua muda kwa sababu ya mkandarasi alikuwa bado hajalipwa hati za malipo. Nimhakikishie Mbunge Mheshimiwa Getere, kwamba barabara hiyo itakamilika, tumeahidi na tunamhakikishia yeye na wananchi wake kwamba hiyo barabara tutaikamilisha kwa sababu tumeshaianza, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kipande cha Barabara cha Mkange – Makurunge ambacho ni sehemu ya barabara ya Afrika Mashariki, tunatambua bado mpaka sasa bado hakijapata mkandarasi, lakini hali yake ni mbaya kutokana na mvua zinazonyesha na kipande hicho kuna Kiwanda cha Sukari cha Bakhresa ambaye ni mlipakodi mzuri wa Serikali.

Je, ni lini Serikali itakifanyia ukarabati ili kiweze kupitika na kumsaidia mwekezaji huyu, tukisubiri kipande hiki kipate mkandarasi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba hii Barabara ya Mkange – Makurunge ilikuwa ina hali mbaya na hasa kutokana na ukweli kwamba ndiyo barabara ambayo inapokea maji mengi kutoka bara, yakiwemo maji ya Mto Wami ambayo maeneo mengi sana hii barabara inakuwa na changamoto, lakini nimwelekeze Meneja wa Mkoa wa Pwani, baada kupungua kwa kipindi hiki cha mvua, aweze kurudi *site*, amuweke mkandarasi ambaye yupo aweze kurejesha mawasiliano na kurekebisha maeneo yote ambayo yameharibika kwa sababu ya mvua ambayo ilikuwa inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Mkange – Makurunge ndiyo kipande ambacho kimebaki kujengwa kwa kiwango cha lami kuunganisha hii barabara ambayo ni ushoroba wa Pwani yote ya Afrika kuanzia kule Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyoongea sasa hivi, Serikali iko inafanya jitihada ya kutafuta chanzo sahihi na cha uhakika kama ilivyo vipande vingine vya kutoka Makurunge kwenda Pangani hadi Tanga ili tuweze kukamilisha hiyo barabara yote ya ushoroba wa kutoka Kenya mpaka Mtwara.

Kwa hiyo, tuna watu ambao tayari tunaongea nao, taasisi mbalimbali za kifedha na zimeonyesha zina nia ya kuweza ku-*support* ujenzi huo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fadhili Ngajilo, swali la nyongeza.

**MHE. FADHILI F. NGAJILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashukuru sana kwa kupewa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wana-Iringa tunashukuru sana kwa kauli uliyoitoa sasa hivi kuhusu ujenzi wa barabara ya njia nne ya Kitonga, lakini pia tulishafikisha wazo zuri kwamba kuna njia nyingine mbadala ambayo ipo kuanzia hapa Ikokoto hapa juu, inapita nyuma ya Kitonga, inatokezea hapa chini eneo maarufu kama *Comfort*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni ipi kauli ya Serikali kuhusu kuwa na njia nyingine mbadala wakati tukiendelea na mkakati wa kujenga barabara zile nne za Mlima Kitonga? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, suala hili tulishalipokea na kama Wizara, wataalam wako wanalifanyia kazi ili kuona kama ile miinuko inaweza kuwa ni nafuu ama ni nafuu kutanua barabara. Kwa hiyo bado tunalifanyia kazi hilo suala na kuona wataalam watashauri nini

kuhusu hiyo barabara mbadala, lakini wakati huo huo tukiwa tunaendelea kujenga Kitonga kwa njia nne.

Kwa hiyo, tayari tumeshalipokea na wataalamu wako kwenye hatua za awali kuona kama inawezekana tukawa na njia mbadala, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kuendelea, naomba niwaletee matangazo ya wageni walioko Jukwaa la Spika; wageni wa Wabunge kutoka Chama cha Mabunge Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika *(CPA);* tunaye Mheshimiwa Refilwe Mtsweni-Tsipane ambaye ni Spika wa *National Council of Provinces* ya Afrika Kusini. *(Makofi)*

Tunaye Mheshimiwa Amos Masondo, Mweka Hazina wa *CPA* Kanda ya Afrika, ahsante sana, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunaye Mheshimiwa Comfort Doyoe, Mjumbe wa Kikosi Kazi cha Mradi wa Hoteli ya Nyota Tano ya *CPA* Kanda ya Afrika, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Modibedi Phindela ambaye ni Katibu wa *National Council of Provinces* ya Afrika Kusini. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Josiah Modiga, Afisa kutoka *NCOP*, Afrika Kusini kwa maana ya *National Council of Provinces*, ahsante sana na karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunaye pia Ndugu Nicole Asimwe ambaye ameambatana na Mweka Hazina wa *CPA* Kanda ya Afrika. Ahsante sana, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni wa Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Mbunge, ambaye ni Naibu Waziri wa Afya ambao ni wafanyabiashara kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Devotha Daniel Mburarugaba ambaye ni mpigakura wake Ndugu Beatrice Justine Kamafa kutoka Kyerwa mkoani Kagera, ahsante na karibu sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 33 wa Mheshimiwa Timoth Geofrey Anyosisye ambao ni wanafunzi wa Shule ya Awali na Msingi *New Montessori* kutoka Jijini Dar es Salaam, ahsanteni na karibuni sana wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ambao ni wafanyakazi wa Shule ya Msingi ya Ilula Malaika kutoka Jijini Dodoma, ahsanteni na karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni 70 wa Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza ambao ni wanafunzi na walimu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Hekima kutoka Bukoba, Mkoani Kagera. Karibuni sana walimu pamoja na wanafunzi. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunaye ndugu Peter Gingiri kutoka Dodoma, Ahsante na karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi na walimu 81 wa *Tanzania Scout Association* kutoka Wilaya ya Ubungo, Jijini Dar es Salaam, ahsanteni na karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 69 wa Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Kampasi ya Tabora, karibuni sana wanafunzi kutoka Chuo cha Umma cha Tabora. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na kabla ya kuendelea Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni ambaye ni Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yuko nje ya Dodoma kwa siku ya leo tarehe 8 Juni na hivyo basi, anayekaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni ni Mheshimiwa David Ernest Silinde. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana, kwa hiyo tumpe ushirikiano Mheshimiwa David Ernest Silinde hapo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, nimwite Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo, Mbunge wa Moshi Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 538

**Kutambua Chama cha Wapagazi *(TAP)***

**MHE. IBRAHIM M. SHAYO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakitambua Chama cha Wapagazi *(Tanzania Association of Posters - TAP)* na kukishirikisha kama mdau muhimu wa utalii nchini?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 20 Disemba, 2025 Wizara ilishiriki katika uzinduzi wa Chama cha Wapagazi *(TAP)* uliofanyika Manispaa ya Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro. Kwa msingi huo, Wizara inakitambua chama hicho ambapo pia imekuwa ikishirikiana nacho katika matukio mbalimbali yanayohusu wapagazi ikiwemo ushiriki wa vikao vya wadau vilivyofanyika Jijini Dodoma pamoja na programu ya mafunzo kwa wapagazi iliyoandaliwa na Wizara kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Utalii Tanzania *(TATO)* yaliyofanyika tarehe 11 Mei, 2026 Jijini Arusha na tarehe 13 Mei, Manispaa ya Moshi Mkoani Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kukubali kuwa mlezi wa Umoja wa Chama cha Wapagazi Tanzania na kumhakikishia kuwa Wizara itaendelea kumpatia ushirikiano katika kutimiza jukumu hilo kwa maslahi mapana ya kukuza sekta ya utalii nchini hususan utalii wa mlima ambapo wapagazi wana mchango muhimu katika kuhudumia watalii wetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo, swali la nyongeza.

**MHE. IBRAHIM M. SHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kwa kuwa Serikali ilishaagiza wapagazi walipwe kwa kupitia akaunti za benki. Je, ni lini Serikali itakwenda kuwakumbusha wamiliki wa makampuni hayo kupokea akaunti hizi za benki za wapagazi na kutokuwalazimisha wao kutumia akaunti zao za wamiliki wa makampuni wanazozitumia?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ni lini Serikali itaweka kanuni na mwongozo wa kuwa na Chama kimoja cha Wapagazi badala ya kuwa na vyama vingi vya utitiri vinavyosababisha vurugu na fujo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Ibrahim kwa namna anavyofuatilia chama hiki na wanachama wake kwa ufanisi mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, anachokisema Mheshimiwa Mbunge kwamba watumishi wale wanalazimishwa kufungua akaunti kwenye benki maalumu. Hili tumelipokea kwa mshangao mkubwa kwa sababu benki zote ni halali na zimesajiliwa rasmi.

Kwa hiyo, nitoe wito tu kwa kampuni hizo wawaachie uhuru watumishi wao wafungue akaunti benki wanazopenda na wapeleke akaunti zao kwa kampuni ambayo imewaajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, ni kweli viko vyama vingi, lakini Serikali inaendelea na utaratibu wa usajili wa vyama hivyo kupitia mfumo. Nadhani na tunaamini kabisa kwamba kupitia mfumo huu hali itaenda kuwa sawia, lakini nitoe wito kwa vyama hivi, wahakikishe kwamba wamejiunga, umoja ni nguvu na utengano ni dhaifu. Wanapokuwa wanapigania maslahi yao ni lazima wawe wamejiunga kwa pamoja.

Kwa hiyo, nitoe wito kwa vyama hivi waendelee kuungana kwa masilahi yao na kwa masilahi ya Taifa letu, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya swali la Mheshimiwa Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara ya Nishati, swali la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini, litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Ghati Chomete, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 539

**Vitongoji Vilivyopatiwa Umeme Jimbo la Tarime Vijijini**

**MHE. GHATI Z. CHOMETE K.n.y. MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza: -

Je, hadi sasa ni vitongoji vingapi vilivyopatiwa umeme katika Jimbo la Tarime Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Salome Makamba, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru na kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* inaendelea na kazi ya kusambaza umeme vitongojini ambapo katika Jimbo la Tarime Vijijini lenye jumla ya vitongoji 500, vitongoji 272 vimeshapatiwa umeme. Aidha, wakandarasi wanaendelea na kazi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji 92 kupitia Miradi ya Kupeleka Umeme Vitongojini Awamu ya Pili A na B, kazi hiyo inatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Desemba, 2029.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitongoji 136 vilivyosalia vitaendelea kupatiwa umeme kulingana na upatikanaji wa fedha na lengo la Serikali kupitia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na Dira ya 2050 ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2030 kila kitongoji kiwe kimefikiwa na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ghati Chomete, swali la nyongeza.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilishasema kwamba vijiji, vitongoji na maeneo yote ambayo yako vijijini yanatakiwa kulipa umeme ili waweze kufungiwa kwa gharama ya shilingi 27,000 lakini mpaka sasa Jimbo la Tarime Vijijini, maeneo ya Nyamwaga, Vijiji vya Sirari na Nyamongo, wanakuwa-*charged* gharama ya kuanzia shilingi 320,000. Hii inapelekea wananchi wenye hali ya chini kwa maana ya kwamba wasioweza kuwa na uwezo wa kufikia gharama hiyo, kupoteza tabasamu.

Je, ni ipi kauli ya Serikali kuhakikisha inawarudishia tabasamu wananchi wa maeneo hayo ili waweze kufikia gharama ya kuingiza umeme katika maeneo yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lingine la pili, tunawapongeza sana Serikali kwa jitihada kubwa za kusambaza umeme katika maeneo mengi nchini.

Sasa ningependa kujua ni mkakati gani mzuri wa Serikali wa kuhakikisha vitongoji vyote nchini vikiwemo Mkoa wa Mara wanaweza kufungiwa umeme ili waweze kupata tabasamu la Dkt. Samia Suluhu Hassan? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kwanza na mimi nianze kumpongeza Mheshimiwa Ghati Chomete, huyu ni simba wa Mkoa wa Mara, simba jike kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwatetea na kuwawakilisha wananchi wa Mkoa wa Mara, hasa wanawake wa Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ghati, sheria inataka na imeshaelekeza, maeneo yote ya vijijini, wananchi waunganishiwe umeme kwa shilingi 27,000. Kwa hiyo, kama kwenye Jimbo la Tarime Vijijini hasa kwenye vijiji ambavyo mmevitaja na vitongoji, wanafanya hivyo, maana yake ni kwamba, watumishi wanakiuka sheria na wanakwenda kinyume na utaratibu. Nawaelekeza *TANESCO* na *REA* walioko katika Jimbo la Tarime Vijijini kuhakikisha wananchi hawa wanapata tabasamu kwa kuunganishiwa umeme kwa shilingi 27,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, lengo na dhamira ya Serikali ni kuhakikisha mpaka inapofika mwaka 2030 vitongoji vyote vinapata umeme. Umeiona dhamira hiyo, mwezi Februari mwaka huu, Mheshimiwa Rais ameidhinisha shilingi trilioni 1.2 tupeleke umeme kwenye vitongoji zaidi ya 9,000 kwa kuanzia na bado

Serikali imeji-*commit* katika bajeti ambayo Waheshimiwa Wabunge mmetupitishia hapa Bungeni, tumeji-*commit* zaidi ya 97% ya bajeti yetu, tunapeleka kwenye miradi ya maendeleo. Nikuhakikishie Mheshimiwa Ghati, Chama Cha Mapinduzi kimeshaelekeza, Dira 2050 imeshaelekeza na sisi Wizara ya Nishati tumeji-*commit* kuhakikisha kwamba, vitongoji vyote vitapata umeme ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuela Kaganda Mtatifikolo, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUELA K. MTATIFIKOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na kwa ridhaa yako ninaomba kwanza kabisa kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuzungumza kwenye Bunge hili Tukufu, nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyekiti wangu wa chama na viongozi wangu kwa ridhaa ambayo wamenipa kupeperusha bendera ya Chama Cha Mapinduzi kwenye Jimbo lile la Isimani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, niwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Isimani ambao wamenipa kura za kishindo, wamenipa imani kubwa kwa kunichagua kwa kura nyingi sana. Ninawashukuru sana wapiga kura wa Jimbo la Isimani na mimi ninawaahidi kwamba nitakwenda kuhakikisha kwamba ajenda zao za maendeleo ninazisukuma ipasavyo kwenye Bunge hili la Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa jinsi ambavyo mlini-*support* kwa kunitia moyo, lakini kwa hali na mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee niwashukuru sana Wabunge Wanawake, wakiongozwa na mama yetu, Mheshimiwa Mary Pius Chatanda ambaye aliweka kambi kabisa jimboni kuhakikisha kwamba ninapata joto la kutosha na ninapata kura nyingi za kutosha na Chama Cha Mapinduzi kinapata kura za kutosha, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Wabunge ambao wanawake pia waliweka kambi pale kwa kuhakikisha kwamba tunashinda kwa kishindo, nawashukuruni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo, ninaomba sasa niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini pia nimshukuru sana mtangulizi wangu Hayati Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru kwa sababu kazi kubwa imefanyika kwenye eneo hili au kwenye sekta hii ya umeme. Kwenye Jimbo langu la Isimani, vijiji 60 vyote vimeshapata, lakini kwenye Jimbo la Ismani vitongoji 236 kati ya vitongoji 290 vimeshapata umeme.

Swali langu ni kwamba je, ni lini Serikali itakamilisha kuleta umeme kwenye vitongoji 54 ambavyo vimebaki? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Emmanuela kwa kushinda kwa kishindo na kupeperusha bendera ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Emmanuela ameapishwa Ijumaa, lakini ofisini kwetu alikuja Jumamosi na Ijumaa hiyo hiyo alirudi jimboni kwake na Waziri Mkuu kwa ajili ya kuwashukuru wananchi. Hiyo inaonesha namna ambavyo Chama Cha Mapinduzi kimechagua Mbunge ambaye anakuja kuchapa kazi na siyo kujifunza kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Emmanuela, sisi Serikali na Chama Cha Mapinduzi, tuna dhamira ya dhati ya kuhakikisha kila kitongoji kinapata umeme mpaka mwaka 2030. Kwa Jimbo la Ismani peke yake, katika vitongoji 54 vilivyobaki sasa hivi tumeshapeleka fedha na wakandarasi kwenye vitongoji 25,

maana yake ni kwamba vitabaki vitongoji 29. Jimbo lako la Ismani ni miongoni mwa majimbo ambayo kabla ya mwaka wa fedha unayokuja, tunatarajia kwamba tutakuwa tumefuta vitongoji vyote na sasa tutakwenda kuzungumza habari ya kupeleka umeme kwenye kaya na sio vitongoji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mohamed Utaly, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED M. UTALY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika majimbo mbalimbali nchini kuna maeneo ya mijini, lakini bado kwa silka na hali za maisha ya watu wake yana hadhi ya vijijini, ikiwa ni pamoja na maeneo ya Tandangongoro, Chikonji, Mbanja na Kitumbikwela katika Jimbo la Lindi Mjini.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wananchi wa maeneo hayo wanaingizwa katika mpango wa *REA* ili waweze kuunganishiwa umeme kwa gharama ya shilingi 27,000 badala ya shilingi 321,000? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mbunge wa Lindi Mjini, amekuwa ni mdau mkubwa sana wa sekta ya nishati na tumekuwa tukishirikiana naye kwa kuhakikisha kwamba tunaimarisha gridi ya umeme katika maeneo ya Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Deo Ndejembi, alishatoa maelekezo wakati anahitimisha bajeti yetu hapa Bungeni na akasema maeneo yote ambayo ni ya mijini lakini yana sura za vijijini, maana yake ni kwamba kwa kiuchumi na mazingira, jiografia maeneo hayo yana sura za vijijini,

wasiunganishiwe umeme kwa bei kubwa badala yake waunganishiwe umeme kwa bei ya shilingi 27,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara mara baada ya kuhitimisha bajeti, tumeanza mkakati wa kukaa na Wabunge ili kuweza kuyabainisha maeneo hayo, tuweze kuyapa fedha na *REA* na *TANESCO* washirikiane kwa pamoja kuhakikisha kwamba wananchi hao wanapata umeme kwa bei ya shilingi 27,000 badala ya shilingi 320,000 na kwenda juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kijakazi Mohamed, swali la nyongeza.

**MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa Serikali kwa sasa ipo kwenye hatua ya kupeleka umeme kwenye vitongoji, ikiwa vipo baadhi ya vijiji ambavyo mpaka sasa bado havijapatiwa umeme kama vile Kijiji cha Songomnara kilichopo Kata ya Pande, Jimbo la Kilwa Kusini.

Je, ni lini sasa Serikali itapeleka umeme kwenye vijiji vilivyosalia kama kijiji hiki nilichokitaja cha Songomnara? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na napenda nimpongeze pia Mheshimiwa Kijakazi kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwakilisha wananchi wake wa Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa rasmi za Serikali, vijiji vyote nchini vina umeme, inawezekana usiwe ni umeme wa Gridi ya Taifa ukawa ni umeme wa *solar*, inawezekana usiwe ni umeme ambao unakuwa *supplied* na kutoka kwenye gridi kama nilivyosema hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba vijiji na vitongoji vyote vinapata umeme ifikapo mwaka 2030 na kwa maana hiyo, kwenye Kijiji hicho Mheshimiwa Mbunge, mimi nitakuja mwenyewe kufanya ziara ili kuweza kuhakikisha kwamba kila maeneo watu wananufaika na uwepo wa umeme mwingi ambao umezalishwa katika nchi yetu, ambao kwa sasa sisi ndiyo tunaongoza kwa *East Africa* kwa uzalishaji wa umeme. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paschal Chinyele, swali la nyongeza.

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Dodoma kwa ujumla wetu, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuimarisha huduma ya umeme katika jiji letu. Hata hivyo, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha umeme wa *REA* wa shilingi 27,000 katika Mitaa ya Mphusu, Chizomoche Kata ya Mbabala, Mitaa ya Chiwondo, Kata ya Nala na Mitaa ya Sabasaba na Karume, Kata ya Mpunguzi pamoja na Mitaa ya Kusenha na Kaunda katika Kata ya Matumbulu? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Chinyele, tumekuwa na mijadala mingi ofisini kwetu kwa ajili ya kujadili namna gani tunaweza kuhakikisha kwenye mitaa mingi ya Jiji la Dodoma, ambayo ina sura ya vijijini inaweza kupata umeme kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotangulia kujibu hapo awali, tulijadili na tukaafikiana kwamba, kwa mitaa ambayo ina mazingira ya vijijini na wananchi wake hawana uwezo kwa sababu wako vijijini, mitaa hiyo Mheshimiwa Waziri alishanielekeza, niketi pamoja na Waheshimiwa Wabunge tuweze kuibainisha, kwa sababu fedha tumeshatenga na

mmetumepitishia Waheshimiwa Wabunge, tuibainishe ili tuweze kupeleka umeme kwa gharama ya shilingi 27,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, na Mheshimiwa Chinyele umeshaleta ofisini kwetu baadhi ya mitaa, pamoja na hiyo ambayo umeitaja. Kama iko mingine ambayo imesahaulika, ofisi zetu ziko wazi kupokea na tuko tayari kuleta umeme kwenye maeneo hayo. Naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Fadhili Chilombe, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na kwa ruhusa yako naomba nitoe maelezo kidogo kabla sijauliza swali langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamekuwa na mijadala mingi sana ya malipo ya shilingi 27,000, kila Mbunge anayesimama anaongelea jambo hili kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo jambo linakanganya wananchi kule. Mwananchi akienda *TANESCO* kuchukua fomu, tunaambiwa fomu ni bure, ili ile fomu irudi *TANESCO,* mwananchi huyo anatakiwa kumlipa mkandarasi hela ya ziada, na hii hela haina kiwango maalum; sehemu nyingine shilingi 20,000, sehemu nyingine shilingi 50,000. Tulishawahi kutoa ushauri Serikalini kwamba Serikali itoe tamko, kwa sababu kimsingi hela ile haina umuhimu na haitakiwi kulipwa.

Sasa nilikuwa naomba kuiuliza Serikali, ni lini itatoa tamko ili kuondoa mkanganyiko huu ambao unaendelea siku zote kwenye nchi hii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kaka yangu, ni Mbunge mzoefu na ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini na hili jambo tulishalishauriana kwenye Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, ili uweze kuunganishiwa umeme, ni lazima awepo mkandarasi kwa ajili ya kuthibitisha kwamba mfumo wa *wiring* uliofanya kwenye nyumba yako uko sahihi na hauwezi kuleta madhara baadaye. Wakandarasi wamekuwa wana-*charge* gharama tofauti tofauti katika kuidhinisha au kudhibitisha ubora wa *wiring* iliyofanyika kwenye nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alishalichukua hili na tunalifanyia kazi ili tuje kutoa mwongozo wa ni gharama kiasi gani, ambayo anapaswa kulipwa mkandarasi ambaye anathibitisha kwamba mfumo wa *wiring* uliofanyika kwenye nyumba una ubora na hauwezi kuleta madhara kwenye nyumba. Nimuahidi Mheshimiwa Mbunge, hili tulishalipokea kutoka kwenye Kamati na tunalifanyia kazi, na muda si mrefu, Mheshimiwa Waziri atakuja na maelezo ya ni gharama kiasi gani inatakiwa kutolewa kwa ajili ya kuidhinisha kwamba ubora wa *wiring* uliofanyika katika nyumba uko sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Isack Copriano, swali la nyongeza.

**MHE. ISACK J. COPRIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri anajua fika kwenye vijiji vyangu vyote kwenye jimbo langu vijiji 63, nguzo maeneo mengi yamepita. Sasa nataka kujua ni lini Serikali itashusha umeme katika Vitongoji vya Olkolili, Imbopong' na Olemama, kwenye maeneo hayo ya vijiji kwa sababu umeme umeshapita?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, awamu ya kwanza wakati tunapeleka umeme vitongojini kuna baadhi ya maeneo ambayo hawakunufaika na umeme, kwa

sababu umeme uliwapita, na hilo tuliliona na Kamati ya Bunge ilitushauri tukafanye miradi wa ujazilizi. Kwenye bajeti hii ambayo mmetupitishia Waheshimiwa Wabunge, tunayo zaidi ya shilingi bilioni 153 kwa ajili ya kufanya mradi wa ujazilizi kwenye maeneo ambayo wananchi *wire* umepita juu hawajanufaika kwa kushushiwa umeme.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Monduli, nikutoe wasiwasi, tutakuja katika maeneo yako na tutaanza kutekeleza miradi hii mara baada ya kumaliza Bunge hili la Bajeti, mwezi wa saba. Nakushukuru sana Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 540

**Hitaji la Umeme Kwenye Mitaa Isiyo na Umeme-Mji wa Tarime**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza: -

Je, lini umeme utafika kwenye Mitaa yote ambayo haina umeme katika Mji wa Tarime?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Jimbo la Tarime Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Tarime una jumla ya mitaa 81 ambapo kati ya mitaa hiyo, yenye umeme ni mitaa 54 na isiyo na umeme ni mitaa 27. Kati ya mitaa 27 isiyokuwa na umeme, mkandarasi anaendelea na kazi katika mitaa 13. Hadi sasa tayari amesimamisha nguzo na anajiandaa kuanza kufunga nyaya. Aidha, Serikali kupitia *TANESCO* imepanga kupeleka umeme

katika mitaa 14 iliyosalia kulingana na upatikanaji wa fedha. Lengo la Serikali ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2030 kila Mtaa nchini uwe umefikiwa na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naishukuru Serikali kwa jitihada ambazo inafanya kuhakikisha kwamba inapeleka umeme kwenye Mji wetu wa Tarime. Ni rai yetu kuitaka Serikali, labda iweze kuhakikisha kabla ya mwaka 2030, walau mwaka 2027 tuwe tumepata umeme katika mitaa yote. Sasa maswali yangu mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mji wa Tarime umekuwa na changamoto ya kukatika umeme hasa nyakati za jioni, kupelekea umeme mdogo au *low voltage*, na hali hii inaathiri shughuli za biashara, uwekezaji na hata ustawi wa jamii kwa ujumla; na kwa kuwa, Serikali ina mradi wa *National Energy Compact* ambao unatarajiwa kutatua hii changamoto, lakini mradi huu unategemea zaidi bajeti za ndani.

Sasa nikataka kujua, kama Serikali ina mpango gani mkakati wa dharura wa kuhakikisha kwamba inatenga fedha za maendeleo nje ya zile bajeti za ndani ili iweze kuharakisha na kuhakikisha kwamba mradi huu unatekelezeka kwa wakati. Kwa sababu, ukitegemea bajeti ya ndani utachukua muda mrefu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Mji wa Tarime unategemea umeme wa njia moja ambao unatoka katika kituo cha kupozea umeme cha Nyamongo ambacho kinaathiri shughuli za uchumi pale ambapo mfumo huu wa usafirishaji wa umeme unapopata matatizo au hitilafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka wa kuweza kutujengea njia mbadala kwa maana *dyness power supply line* ambayo itakuwa ni mbadala,

kama ile nyingine ikipata matatizo ili kuhakikisha sasa, Mji wetu wa Tarime unapata umeme nyakati zote kuliko ilivyo hivi sasa hivi unaweza kuwa unapata umeme, lisaa limoja umeme umekatika. Ikizingatiwa Mji wa Tarime ni mji wa kimkakati, ni lango kuu la uchumi, uko mpakani kwa maana ya biashara, utalii, madini na uwekezaji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mbunge wa Jimbo la Tarime Mjini, amefuatilia sana kutatua changamoto ya kukatika katika kwa umeme katika Jimbo la Tarime, Tarime Mjini na Tarime Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali hili liliulizwa wiki kadhaa zilizopita na baada ya hapo, sisi ofisini tuliketi na kuangalia kwa nini umeme unakatika sana pale Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, uniruhusu nielezee *background* kidogo; pale Tarime, kituo chetu cha kupoza umeme cha Nyamongo kina uwezo wa kupoza umeme na tunaweza kupata kama megawati 70, lakini Tarime peke yake, inatumia megawati 38, megawati 30 kwenye ile migodi mikubwa miwili na megawati nane kwa Tarime Mjini, jambo linalofanya Tarime peke yake kutumia zaidi ya nusu ya umeme wote unaozalishwa pale Mkoa wa Mara. Umeme wote wa Mkoa wa Mara zaidi ya nusu unatumika Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara, tumechukua *affirmative actions* kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto hii, kwa sababu Tarime ni sehemu ambayo kweli kama ulivyosema, ni lango la kiuchumi na ni eneo la kimkakati kuna migodi mingi. Tumechukua hatua zifuatazo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, Mheshimiwa Mbunge; Umeme unaokwenda kanda ya ziwa, unasukumwa kwa msongo wa kilovolti 220, jambo hilo *obvious* kutakuwa kuna *low voltage* zitatokea mara kwa mara. Nimewaelekeza wataalamu wetu

kuhakikisha kwamba wanajenga kwa haraka *line* ya msongo wa kilovolti 440 kutoka Dodoma, Singida kwenda Shinyanga, itasaidia sana ku-*feed* hiyo *line* inayoenda Mkoa wa Mara. Hiyo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tunao mradi mkubwa sana wa kutoa msongo wa kilovolti 440 kutoka Chalinze kuja Dodoma, hiyo itasaidia kupunguza umbali wa *line* pia. Mheshimiwa Mbunge, umeshauri vizuri, kwamba pale Tarime ile *line* inayokwenda kwenye maeneo ya migodi ambayo inatumia umeme mwingi inasababisha *voltage dips and sags,* tunaitoa *line* nyingine *(alternative line)* kuweza kuwasaidia wananchi wa Tarime wasipate kukatika katika kwa umeme, wakati maeneo ambayo yana uzalishaji mkubwa au yanatumia umeme mwingi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge ni suala la muda tu, utuvumilie, tunakimbiza kazi hii usiku na mchana ili kuhakikisha lengo letu la kuwahudumia Watanzania na umeme utumike kiuchumi linafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tinnar Chenge, swali la nyongeza.

**MHE. TINNAR A. CHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni sera ya Serikali kupeleka umeme kwenye taasisi za umma, na kwa kuwa Shule ya Sekondari ya Bunamhala iliyopo Mtaa wa Songambele, Bariadi, hakuna umeme. Je, ni lini Serikali itapeleka umeme kwenye shule hii ili wanafunzi waweze kusoma? Ninakushukuru *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze mama yangu Mheshimiwa Tinnar Chenge, umekuwa na bidii sana na umetushauri vizuri sana kuhakikisha kwamba, Mkoa wa Simiyu kwa ujumla unapata umeme wa uhakika, lakini pia tunafikia taasisi nyingi za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, mpaka kufika Ijumaa ya wiki hii, hiyo shule itakuwa tayari imeshapata umeme. Ninamwelekeza Meneja wa *TANESCO* Mkoa wa Simiyu kuhakikisha taasisi zote za Serikali zinapata umeme ili tija ionekane ya uwekezaji katika taasisi hizo, maana sisi Serikali ni moja na tunazungumza pamoja. *By Friday* wiki hii shule itakuwa imeshapata umeme. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Karatu tuna vitongoji 266 na kati ya hivyo tayari vitongoji 191 vina umeme. Tunaishukuru Serikali na kuipongeza kwa kazi kubwa ya kupeleka umeme. Bado tuna vitongoji 75 hatujapata umeme. Je, ni lini vitongoji hivyo vitafikiwa na huduma hiyo ya umeme?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kwanza kwa kufuatilia na kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma nzuri ya nishati ya umeme. Mheshimiwa wewe ni jembe kweli kweli, mimi ninakufahamu ni dada yangu. Mheshimiwa Paresso mpaka mwaka 2030, hivi vitongoji vyote 75 vilivyobaki, vitakuwa vimeshapata umeme. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Regina Mikenze, swali la nyongeza.

**MHE. REGINA H. MIKENZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Mimi napenda kuuliza, kwa kuwa shughuli za uchimbaji madini zinategemea sana nishati ya umeme.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inapeleka umeme wa uhakika kwa wachimbaji wadogo wadogo wa madini wa Mkoa wa Geita? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na nampongeza Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kwa ushauri mzuri anaoendelea kutupa sisi Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Mbunge, Bunge hili Tukufu kwanza tunalishukuru sana. Tulikuja katika Kamati tukiwa na mapendekezo ya kupata fedha kwa ajili ya kupeleka umeme kwenye migodi midogo midogo, tukiwa tunachambua kwamba migodi ile inahitaji nishati hiyo ili uzalishaji wao wa madini uwe wa gharama nafuu waweze kupata faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili Tukufu, lilitupitishia zaidi ya shilingi bilioni 20 ili tuweze kupeleka umeme kwenye migodi midogo midogo. Hivi sasa tunasubiri mara baada ya Bunge hili kumalizika, tuanze kukimbia mchakamchaka na kuwapelekea wananchi wanaofanya kazi kwenye migodi midogo midogo, umeme wa uhakika waweze kuzalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, tutaketi pamoja na ninyi Waheshimiwa Wabunge na wawakilishi wa Mkoa wa Iringa, tuweze kubainisha maeneo haya, ili kwa kuanzia, tuweze kupeleka umeme katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Ramadhani Hamza Singano, swali la nyongeza.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza niipongeze Serikali yetu, katika vitongoji 673 vya Bumbuli, vitongoji 408 vina umeme na 117 vinaendelea kupatiwa umeme. Ni lini vitongoji 148 vitatekelezwa navyo kupata umeme?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Mbunge na kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge, katika historia ya nchi hii, kwa mara ya kwanza, tangu Bunge hili limeanza, mwaka huu ndiyo tumesaini mkataba mkubwa wa kupeleka umeme kwenye vitongoji vingi kuliko miaka yote.

Waheshimiwa Wabunge, wote mtakubali, wote mlipewa lile jedwali la namna ambavyo tunapeleka umeme kwenye vitongoji vyenu. Sasa hivi tuna shilingi trilioni 1.2 kuhakikisha tunapeleka umeme kwenye vitongoji 9,002 na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa kushirikisha wadau mbalimbali, kuhakikisha vitongoji vilivyobaki chini ya 30% vilivyobaki vinakamilika kabla ya mwaka 2030. Waheshimiwa Wabunge niwatoe wasiwasi, vitongoji vyote vilivyobaki vitapata umeme kabla ya mwaka 2030 na hiyo ni dhamira ya Mheshimiwa Rais, na hayo ni ahadi ya wananchi kupitia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Phillipo Mulugo, swali la nyongeza.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Chunya na Wilaya ya Songwe kwa ujumla, upande wa wachimbaji wadogo, umeme upo lakini ule umeme ni mdogo kiasi kwamba hayasukumi makarasha vizuri pamoja na wachimbaji wote wakubwa kwa migodi ya kuwekea *CIP,* yaani maana yake, umeme ukiwashwa Chunya, ukiwashwa Saza, ukiwashwa Makongolosi, Mbangala, Mwaoga, kote, yanaweza yakafanya kazi makarasha 100, makarasha mengine 100 yamebaki bila umeme. Yaani umeme ni mdogo sana. Nini tatizo la Serikali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na nafahamu Mheshimiwa Mulugo tumeshazungumza kuhusiana na changamoto ya umeme mdogo kwenye maeneo hayo ya wachimbaji anayoyataja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa, miaka kumi iliyopita, eneo lile lilikuwa halina uchimbaji mkubwa kama unaofanyika sasa hivi, na wachimbaji hawakuwa wengi kama ilivyo sasa hivi. *Obvious*, lazima umeme ulioko sasa hivi uwe ni mdogo kuweza kuhudumia mahitaji makubwa yaliyoko pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anafahamu tuna Mradi wa Taza kule kwa ajili ya kupeleka *line* kubwa ya umeme ambayo ita-*cross* Chunya na kwenda Zambia. Mradi ule utaenda kutusaidia sana kupunguza changamoto ya *low voltage* katika maeneo ya Mbeya na Chunya.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, tuwe na subira kidogo, tunakwenda kuimarisha upatikanaji wa umeme kule na tunafahamu umuhimu wa wachimbaji wadogo katika kuchochea uchumi wa nchi yetu. Nikutoe wasiwasi, jambo hilo litakamilika na mradi unaendelea kwa kasi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwetu na majibu kutoka upande wa Serikali. *(Makofi)*

Kuna matangazo hapa kutoka kwa Meneja wa *Bunge Sports Club,* Mheshimiwa Festo Richard Sanga; itakumbukwa siku ya Jumamosi kulikuwa na mechi ya kirafiki kati ya *Bunge Football Club* pamoja na Albino Tanzania na matokeo ya mchezo huo ilikuwa ni kama ifuatavyo: -

Bunge walipata magoli matatu na Albino Tanzania pia magoli matatu. Kwa upande wa Bunge, magoli yalifungwa na Waheshimiwa Wabunge wafuatao: Mheshimiwa Mohamed alifunga goli moja, Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Meneja wa *Bunge Sports* amefunga magoli mawili. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaipongeza timu yote ya Bunge kwa kushiriki mchezo huo wa kirafiki. Pongezi nyingi kwa Meneja wa *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa Sanga kwa magoli mawili pamoja na Mheshimiwa Mohamed. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hili, naahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 5.05 Asubuhi Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 9 Juni, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA